mafundisho

ya Eklezya Katolika

# Jamaa Takatifu



# PREFACE

Tout restaurer dans le Christ, voilà l'esprit qui nous a guidé dans l'approche de l'expérience chrétienne qu'est la jamaa !

L'accès au Père ne peut s'obtenir que par l'union avec le Fils !

C'est pourquoi nous invitons les membres de la jamaa de rester en communion avec les Evêques qui sont les successeurs des apôtres. C'est par eux et avec eux que, œuvrant dans un esprit de dialogue, ils connaîtront cette plénitude de joie avec le Père !

+ [signature] le 24.8.7[illegible]

INTRODUCTION.

Voici une première rédaction, provisoire, des mafu
disho de la Jamaa. Il va sans dire que ce texte n'est
parfait, loin de là! D'ailleurs les mafundisho par exc
lence de la Jamaa demeureront toujours l'Evangile lui-
même.

Ce que nous présentons ici suit de près un texte o
ginal qu'un groupe de Baba ont écrit, en 1969, à la de
mande de Mgr Kabanga. Ce texte a été maintenant corrig
en sorte qu'il puisse satisfaire aux exigences de la d
trine catholique.

Ces 'mafundisho' ne sont pas toutes les mafundisho
qui se donnent dans les réunions de Jamaa; et l'ensemb
réuni ne veut pas du tout être un livre scolaire dont
leçons se donnent selon un cycle bien défini.

Les passages d'Evangile ont été choisis selon un b
précis que le candidat doit atteindre pour chacune des
étapes, au cours de son cheminement pour DEVENIR JAMAA
conversion au Christ - union du foyer - don, épanouiss
ment au service de l'Eglise.

Les 'mafundisho' ne sont donc pas la Jamaa; mais
la mesure où quelqu'un est uni au Christ qui l'unit au
autres (et le Christ unit le mari et la femme et les
fants dans leur propre foyer d'abord), alors cette pe
sonne devient Jamaa. C'est là l'idéal à réalise puisqu
Dieu, qui est Jamaa (Trinité), nous a créé a son imag
et le modèle à imiter est le foyer de Nazareth, de Jo
Marie et Jésus.

Les 'mafundisho' sont un moyen; et ce qui compte
sentiellement, c'est la véritable conversion, le reto
nement intérieur dans la rencontre avec le Christ. Et
cheminement peut être plus ou moins long selon les in
vidus, 5 ou 8 ou 10 ans... et encore! Ce qui est le p
important, c'est la croissance des personnes dans leu
vie d'union avec le Christ, c'est le changement de vi
C'est pourquoi les 'mafundisho' ne sont pas la soluti
miracle au problème-Jamaa.

Cette présentation des 'mafundisho' est un ex
d'ouverture et de travail de collaboration constr
entre les chrétiens Jamaa et la Hiérarchie , trav
patience, lent et parfois ardu, pour l'édificatio
Royaume du Christ. Elle est en même temps une inv
au dialogue pour tous les membres de la Jamaa, da
esprit d'humilité, d'acceptation des voies de Die
nous mènent toujours à une purification, à un dét
intérieur plus parfait, pour adhérer, comme le Ch
à la Volonté du Père.

La rencontre avec les Pasteurs, si elle nait
sir d'entente et de vraie Charité, ne pourra que
des fruits excellents pour l'Eglise. D'ailleurs,
ce même Esprit, lors de leur réunion de Likasi, e
vier '73, les Evêques prenaient des mesures où il
traient leur volonté d'intégrer dans l'Eglise, d
tout ce qui pouvait être retenu de cette expérien
vie chrétienne que veut être la Jamaa, selon le c
de l'Apôtre: "N'éteignez pas l'Esprit; mais véri
ce qui est bon, retenez-le." I Th.5,19

C'est ainsi qu'avec ces 'mafundisho' nous esp
servir. Et l'Esprit de Dieu, qui est toujours à
en nous et autour de nous, saura inspirer à tous
chacun les attitudes à prendre dans ce travail d
haleine, qui est à la mesure de Dieu seul : la c
tion du Corps du Christ, jusqu'à sa stature parf
et où chacun de nous reçoit sa part à apporter.

Nous aimerions recevoir vos commentaires, re
et suggestions, quant au contenu et à la présent
en vue d'une éventuelle réimpression. Merci!

# Reglement d'ordre intérieur de la Jamaa.

## Ingilio.

Tangu kuundwa kwake, kundi lile la JAMAA halikuandika mafundisho na kanuni zake. Lakini tukiona lazima za wakati wa sasa, na tukiogopa kurudi tena mu makosa na fujo za zamani, 'Comité central' ya kundi la Jamaa inatunga, kwa jina la waJamaa wote, kanuni zifuatazo :

1) Baba na Mama wa Jamaa anapashwa kujua kama yeye ni kwanza Mkristu kama wakristu wengine wote. Kwa hiyo anapashwa kuishi pamoja na wakristu wote katika masaidiano na masikilizano ya mapendo.

2) Kila mjamaa anapashwa kufanya kazi ya kitume mu 'paroisse' yake :
   - kufika ku mikusanyo ya 'quartier' na kutumika kazi atakayopewa na mkubwa wa 'quartier'.
   - kusaidia kazi ya kufundisha wakatekumeni, wa ndoa, wa kukomunika, na vivi hivi, mu paroisse.

   Basi, kwa kuweza kutimiza vizuri kazi hizi zote, ni lazima kufuata mafundisho mbalimbali yanayoletewa mu 'paroisse', kama vile :
   - mafundisho ya Biblia,
   - mafundisho ya wakatekista.

3) Mjamaa wa kweli anapashwa kufika ku mikusanyo yote na kufuata vizuri mafundisho ya Jamaa. Mjamaa mwenyi kubaki tu ku nyumba yake ataangaliwa kama mwenyi kuisha kutoka katika kundi, na anabaki rafiki tu.

4) Mjamaa anapashwa kupenda pia makundi mengine ya wakristu na kuheshimu mafundisho yao. Tusizarau basi wengine na kuangalia kundi lao kama ni la bure.

5) Baba ao mama wa Jamaa anapashwa kuonyesha mifano yenyi kupatana na mafundisho anayopewa katika kundi. Ni kusema, kuonyesha mifano na mwendo mzuri mbele ya watoto wetu nyumbani na pia kwa watu wote.

6) Baba ao mama mwenyi kuonyesha mifano mibaya atashauriwa na wababa wa 'paroisse' yake. Ikiwa anaongeza vitendo vyake vibaya, ataweza kupata mashauri kwa wa'membres' wa 'comité central', mpaka atakapogeuza mwendo na mifano yake.

7) Mjamaa aliyetengana na Eklezya kwa mapenzi yake yeye mwenyewe, akitaka kurudi katika kundi la Jamaa, atapo kelewa. Lakini atapashwa kukubali na kutimiza mapashw yake mbele ya wakubwa wa Eklezya na kufuata kanuni za kundi la Jamaa.

8) Baba ao mama wa Jamaa mwenyi kutoka mu 'paroisse' yak na kwenda ku 'paroisse' nyingine, ao wageni wanaotoka fasi ya mbali wanapashwa kuonyesha barua ya wababa na wamama wa fasi ile wakitaka kukubaliwa na kutiwa kati nyumba (njia) ile ya mafundisho wamepokwisha kuifikia kama sivyo, watakubaliwa kama wapya na watatiwa mu ma fundisho ya wale wanaoanza mafundisho ya Jamaa.

9) Masaidiano katika kundi la Jamaa yanapashwa kuwa kama vile zamani, bila kuangalia tu ndugu, kabila, cheo ao mali; lakini baba ao mama wa Jamaa anapashwa kumsaidi mwengine kwa mapendo ya kundi la umoja.

10) Dini ndiyo shina la heshimu na adabu. Kumbe katika ku nywa, kula na katika karamu, baba ao mama wa Jamaa an pashwa kuwa mwenyi heshima na adabu. Vilevile kama un tembelea mjamaa mwenzako, piga hodi mbele ya kuingia nyumbani mwake, ili upate kukaribishwa na kupewa fasi ya kukaa.

11) Mafundisho ya Jamaa yanapashwa kufundishwa tu ku 'pa roisse' ao mu fasi nyingine itakayochaguliwa na kujul shwa na padri msimamizi wa 'paroisse'.

12) Padri msimamizi wa 'paroisse' ao mwengine anaweza kuh zuria mafundisho ya Jamaa; kama hana wakati, atawaac waJamaa kufanya mafundisho, pasipo kizuio, akiwatumai wale wanaofundisha.

13) Wanani wataweza kufundisha ?

a.- Kila baba ao mama wa njia tatu aliyechaguliwa na n tatu wa 'paroisse' yao pamoja na 'curé' wao, ni wa wanaoweza kufundisha.

b.- Katika mafundisho ya wote, baba ao mama yeyote, ha asiye wa njia tatu, anaweza kufundisha.

c.- Padri anaweza pia kufundisha katika mafundisho, ha zuru ya njia gani.

14) Mafundisho ya Jamaa ni mafundisho ya Mungu, haizuru y njia gani. Kumbe tusiuzishe mafundisho kwa mali ao kw kitu kingine. Tuyapane kwa bure, pasipo kuomba kitu k wababa na wamama tunaowafundisha.

15) Kwa kuwa mafundisho ya Jamaa ni yenyi kugawanyika katika vipande vitatu, wababa na wamama wenyi kufundisha wanapashwa kutengeneza pamoja na 'Curé' wao 'programme' ya mafundisho. Ni kusema: siku, saa na fasi.
Kwa mfano:-mafundisho (général) ya wote pamoja, siku yao.
-mafundisho ya vipande, katika nyumba mbalimbali za 'paroisse'.

16) Baba ao mama anayekuwa tayari kwa kuingia katika njia yake ya kwanza yupo na uhuru wa kuchagua baba ao mama yake msimamizi. Asilazimishwe kuchagua baba ao mama fulani tu.

17) Wababa na wamama walio tayari kwa kupata njia yao ya kwanza ao ya pili ao ya tatu wanapashwa kuonyeshwa katika mkusanyo wa wababa na wamama wa njia tatu unaofanyikwa mara moja kila mwezi. Humo watapewa mashauri yenyi kuelekea njia yao.

18) Nani ana ruhusa ya kuingiza njia?
Kazi ya kuingiza wababa na wamama katika njia ya kwanza, ya pili ao ya tatu ni ya Padri peke yake.

19) Ikiwa ni fasi pasipo Padri, baba na mama wa njia tatu waliopata ruhusa kwa Padri wanaweza kuingiza wengine katika njia ya kwanza ao ya pili tu. Njia ya tatu ni Padri tu mwenyi uwezo wa kuingiza wababa na wamama. Hata akiwa mbali, watamchunga ao watamfuata.

20) Baba ao mama asiyeweza kufanya vizuri kazi yake yote ya kitume mu 'paroisse' wala mu 'quartier' kwa sababu anafundisha mafundisho katika kundi, atapashwa kutumika kwa ajili ya Eklezya mzima kwanza; na 'Curé' akimwambia, basi atafanya tu kazi ya paroisse. Baba wa Jamaa wa kweli hawezi kuacha (kusura) kazi ya 'paroisse' anayopewa na 'Curé' yake.

N.-B. Kanuni hizi si zote, kumbe zinaweza kuongezeka na kubadilishwa, ikiwa lazima.

Fait à Lubumbashi, le 9/6/74

Approuvé et signé par
Mgr KABANGA.

" Ingieni kwa mlango mwembamba;
kwa sababu mlango ulio mpana
na njia yenyi nafasi kubwa,
ndiyo inayopeleka katika upotevu.
Watu wanaoingia kule wapo wengi.
Bali mlango wa Uzima ni mdogo tu,
na njia ya kwenda mahali pa Uzima ni nyembamb
sana.
Haipatikani na watu wengi. "

Mateo 27,13-14

Mafundisho ya Jamaa .

+ NJIA YA KWANZA +

## INGILIO .

### Mafundisho kwa kuzaa mtu katika Jamaa.

Mtu yule hatutamwambia neno hata moja ya mafundisho yenyewe ya Jamaa. Tunaanza na urafiki tu, tukiulizana na kuonyeshana juu ya mawazo yetu vile tuko nayo katika umuntu wetu.

- Wewe unataka nini? Ninataka hivi.
- Wewe unatafuta nini? Ninatafuta hivi...

Kila siku, tunapima kwanza kujuana na kusikilizana juu ya mawazo ya umuntu wetu, kama ni uzima, uzazi na mapendo; kumsikilizisha mtu mifano ya vitendo, vilema, mapendo, huruma, uvumilivu, masikilizano na masaidiano; kuleta mifano ya kuelekeza mtu katika njia ya Mungu, apate kugeuka na kujitolea kabisa, kuwa mwenyi Imani ya kweli ya mtu wa Mungu.

Mafundisho haya yataweza kudumu muda wa miezi mitatu ao zaidi, kadiri ya kugeuka kwa mtu mwenyewe. Kiisha kutambuka kama baba ao mama wanageuka kweli, ndiyo pale tutawapa mafundisho yenyewe ya Jamaa, katika kundi, pamoja na wababa wengine. Akiwa mpagani, tutampeleka kwa Padri wa Paroisse, kusudi afuate mafundisho ya wakatekumeni, ili apate Ubatizo. Akiwa mkristu bila ndoa ya kikristu, tutampeleka vilevile kwa Padri.

°=°=°=°=°=°=°=°=°=°=°=°=°

## MAFUNDISHO YA NJIA YA KWANZA .

Maana ya "Njia ya kwanza". Njia ya kwanza ni ukumbusho wa Ubatizo wetu, kwani mtu, kiisha kubatizwa, aliungana na Mungu katika mawazo yake yote tatu : Ubaba wake, Umwana wake na Umoja wa Mapendo yake. Hii ni njia ya kwanza ya mtu kwa Mungu wake, na msinji wa njia nyingine yote, na maendeleo ya mtu katika njia ya Jamaa ya Mungu.

### 1/ JAMAA NI NINI ?

Jamaa ni kundi moja la wakristu, katika makundi mengine ya Eklezya Katolika; wakristu hawa wanajikaza kwa kujikumbusha mafundisho ya ukristiani wao, chini ya uongozi wa Papa wa Roma, Maaskofu na Mapadri. Ni umoja wa wale wanaoishi katika masikilizano, masaidiano na mapendo.

Mifano : bwana na bibi na watoto, kizazi fulani, société fulani, na vivi hivi... Tunasikia hapa kama kuna maana ya jamaa ya namna mbalimbali. Lakini Jamaa tunayotaka kusema ni ile inayokusanyika kwa jina la Kristu na kwa kufuata mfano wa nyumba ya Nazareth; ndiyo kundi la Jamaa Ntakatifu.

## 2/ JAMAA INATOKA WAPI ?

Jamaa ni kundi linaloanza leo? Hapana. Mungu ni mmoja. Lakini katika Mungu mmoja, kuna nafsi tatu : Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Maana yake, Mungu ni Jamaa na mfano wa jamaa yote ya dunia. Basi mawazo ya kundi letu la Jamaa hayatoki kwa mtu, lakini yanatoka kwa Mungu mwenyewe aliye JAMAA.

## 3/ JAMAA KATIKA MAWAZO YA MUNGU.

Tangu milele Mungu alikuwako; alikuwa Jamaa katika Umungu wake : Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Hakukuwa na lazima ya kitu; alikuwa tayari: wa uzima, na uzazi na mapendo. Alikuwa wa uwezo na nguvu yote, mtajiri, na furaha tele.

Hakukuwa wala mbingu, wala dunia, wala nyota, wala mwezi na jua; hakukuwa kitu chochote.

Kwa mapendo yake, Mungu aliwaza kuwa na kiumbe atakachoungana nacho na kujitolea vyake vyote. Ni pale Mungu akamwaza mtu, na mara akawa naye katika mawazo yake. Na yule akuwa mtu mawazo : hakuwa mwanaume wala mwanamke, mtoto wala mkubwa, kijana wala mzee. Hakuwa na rangi wala na kabila, mzungu wala mweusi... Alikuwa mtu mawazo. Mungu alimchunga mpaka katika mawazo yake na kuwa umoja kabisa katika ubaba wake, katika Umwana wake, na mapendo yake yote. Akamtakia uzima, uzazi, mapendo na furaha yake yote.

## 4/ JAMAA YA MBINGU : WAMALAIKA.

Mungu alipokwisha kuwa na mtu katika mawazo yake, akakumbuka kuumba tena viumbe vingine vyenyi roho tupu, pasipo mwili, ambavyo vitafanana na Yeye mwenyewe, na vitakavyo mwabudu na kumheshimu na kumwimbia siku zote Muumbaji wa hata vitakavyompenda na kutimiza mapenzi yake : ni wamalaika. Kama vile Mungu ni umoja, ni mapendo na jamaa katika Yeye mwenyewe, vivyo hivyo alitaka umoja wa kweli kwa wamalaika.

Mungu aliwaweka wamalaika katika mbingu wapate kutimiza kazi yao ya kumheshimu na kumwabudu na kumwimbia, na kuwa naye kitu kimoja.

## 5/ JAMAA YA NAZARETH, DUNIANI .

Mungu alipokwisha kuumba Jamaa ya mbingu (wamalaika), akawaza tena kushusha Jamaa katika dunia. Ni pale aliumba Jamaa ya kwanza, ya nkambo zetu Adamu na Eva. Hawa lakini wakakosa kumtii Mungu wao, wakavunja umoja kati yao wenyewe na kati yao na Mungu. Na hivi, Jamaa ile ya kwanza duniani iliharibika.

Lakini Mungu wa huruma yote hakuchoka kuwahurumia viumbe vyake.

Ni hivi alijenga Jamaa nyingine katika nyumba ya Bikira Maria na Yosefu mtakatifu, pa Nazareth; na katika nyumba ile, alimshusha Mwana wake wa pekee, Bwana wetu Yesu Kristu.

Jamaa ile ilikuwa ya kweli na mfano kwa watu wote, kwa sababu ilitimiza mapenzi yote ya Mungu kwa kuchunga umoja wao kati yao, na umoja wao na Mungu. Katika nyumba ile, kulikuwa masikilizano ya kweli; kati yao hakukuwa mkubwa wala mdogo, waliishi kama waana wa Baba mmoja, Mungu mwenyewe.

Na sisi wote pia - baba, mama na watoto - tunapashwa kufuata mfano huo wa Jamaa ile ya Nazareth, katika nyumba ya Yosefu na Maria, kusudi tuwe mfano kwa wenzetu.

## 6/ JAMAA YA BWANA YESU NA MITUME .

Bwana Yesu alipoeneza miaka makumi matatu, na alipoona kama nyumba ya Bikira Maria na Yosefu ni tayari, akaanza sasa kazi aliyotumiwa kuitimiza duniani, ya kutangaza ukombozi wake.

Ni pale alichagua mitume wake kumi na wawili, watu wa mbalimbali, akawaunganisha na kuwafanya kuwa Jamaa yake. Halafu akaanza kuwafundisha namna ya kusikilizana, kusaidiana na kupendana kati yao, kama vile Mungu anavyowapenda.

Katika Jamaa hii, Bwana Yesu aliwafundisha hasa na mifano yake, kukaa pasipo chuki,wala masimango, wala hasira, wala majivuno kati yao, na hata kwa watu wengine. Sababu alijua ya kama kazi watakayobaki nayo itakuwa ya lazima sana : kufundisha na kuongoza dunia nzima.

Basi sisi, wababa na wamama, tunapashwa kutii na kushik
amri za Eklezya Katolika, kwani ndiyo njia yetu kwa kuf
mbinguni. Kumbe msiwaze, wababa na wamama, ya kama Jama
ni kitu kingine kinachoachana na Eklezya ntakatifu ya Mu
gu. Hapana.

## 7/ MAFUNDISHO YA UMUNTU WETU.

Kwa kumtumikia mtu kadiri ya mapenzi ya Mungu mwenyewe, lazima kwanza tujue umuntu wetu.

Mtu ni nini? - Mtu ni mawazo, kama vile alivyowazwa na gu; hakuwa mwanaume wala mwanamke, hakuwa na rangi, hak na kabila.

Mifano: - Katika safari, tukifika fasi yenyi njia inayo roka sana, yapata kilometri hata ine, na kule mbele yetu, mbali sana, kukiwa mtu anayekuja, tutaona tu kama mtu yule anakuja, lakini hatu jua kama ni mwanaume ao mwanamke, mzee ao kij hata rangi yake; isipokuwa kama tunakaribiana naye, pale tutafahamu tofauti yoyote.

- Nikiwa kitako nyumbani, nitawaza ku kazi, ku shamba, ku Likasi, hata kwetu mjini, na nitao ginsi mji upo katika mawazo tu, lakini mwili wangu upo hapa tu L'shi na ndani ya nyumba ya

Mifano ni mingi sana, hatutaweza kuandika yote. Kumbe, wababa na wamama, tunasikia vile mtu ni mawazo. Ukimfan zia mabaya ao mema, ni wewe mwenyewe unayejifanyizia!

## 8/ MAWAZO YA MTU.

Mtu mzima yupo na vipande viwili: roho na mwili. Sababu akikosa mwili si mtu, ila ni malaika; na akikosa roho, mtu, ila ni nyama ao mti.

Mtu ana mawazo mangapi juu yake mwenyewe?
Mtu yeyote, katika mawazo juu yake mwenyewe, ana mawazo makubwa matatu; ndiyo mawazo ya kutafuta :

- Uzima wa mwili na wa roho.
- Uzazi wa mwili na wa roho.
- Mapendo ya mwili na ya roho.

Mungu, kwa ubaba wake, ametupatia uzima; kwa umwana wak Mungu ametupatia kuzaliwa; na kwa umoja wake, Mungu ame patia mapendo yake.

Uzima

a) Uzima wa mwili unaonekana katika matendo: kutembea, kula, kusema, kucheza, kuimba, kutumika, na vivi hivi. Tunachunga uzima wa mwili tukiepuka hatari, tukijichunga vema, tukikula, tukijitunzisha kama tupo wagonjwa... Hatuchungi uzima wa mwili tukitumia dawa ya kipuuzi. Uzima wa mwili ni wa kipande tu; uzima wa mwili upo na mwisho... Tunajua lakini ya kama kuna ufufuo wa mwili!

b) Uzima wa roho : ni kuwa na hali ya neema ya utakaso; tunaipata katika mafundisho ya Mungu, sakramenta, sala. Tunachunga uzima wa roho tukiepuka njia zote zenyi kutusukumia katika zambi. Uzima wa roho ni wa milele kwani hauna mwisho. Lakini zambi inaweza kuiharibisha na kuiua hali ile ya neema ya utakaso.

Uzazi

a) Uzazi wa mwili ni kuzaa mtoto kwa mwili. Tunapata uzazi kwa Mungu peke yake. Hatuwezi kuutafuta katika mambo ya upuuzi; kwa mfano: kuaguza, kuvunja ndoa na kutafuta mwengine kwa kuzaa naye, kuongeza bibi wa pili, kuomba mizimu ...

Kumbe, wababa na wamama, namna nzuri ya kutafuta uzazi ni kumwomba Mungu, na kutunzwa na dawa nzuri ya mganga tukiwa wagonjwa.

Uzazi wa mwili ni wa kipande, kama vile uzima wa mwili.

b) Uzazi wa roho ni kumzaa mtu ku roho, maana yake, kumsaidia apate kugeuka na kuzaliwa mtoto wa Mungu katika Ubatizo akiwa mpagani, ao apate kufufuka katika uzima ule wa Mungu kwa sakramenta ya Utubio akiwa mkristu aliyeacha njia yake ya ukristiani. Uzazi wa roho hauna mwisho wala kipimo, ni wa watu wote. Tunapata uzazi wa roho kwa mafundisho ya dini ya Mungu, kwa matendo na mifano mizuri ya kikristu, na kwa sala zetu.

Basi, wababa na wamama, kwa kutaka tuwe na uzazi huu, tunapashwa kujikaza kuwa mfano kwa wengine. Tuonyeshe umoja wetu : baba na mama na watoto, Padri na wakristu wote, na Mungu atatupa uzazi wake na atatusaidia tusiuue tukiisha kuupata, lakini tuuchunge na kuukomesha.

Mapendo

a) Mapendo ya mwili ni kuheshimu, kuchunga, kutunza na kulisha mwili wetu, hata ule wa watu wengine. Mapendo haya nayo ni ya kipande.

Kumbe, wababa na wamama, kupenda ni kujitolea kwa kuwas dia wengine, pasipo kuangalia faida yetu tu. Hapa dunia watu wanatafuta zaidi mapendo ya mwili kuliko mapendo y roho, sababu mwili ni kitu wanacoona kwa macho.

b) Mapendo <u>ya roho</u> ni kumtakia mwenzako ile yote una taka wakufanyizie wewe. Mapendo haya hayana uchaguzi, u bila, undugu ao urafiki; hayaombi malipo ao kujionyesha Mapendo ya roho ni zawadi kwa kuweza kuhurumiana, kusik lizana na kusaidiana, katika upole, unyenyekevu, kwa ku heshimu mtu mawazo, bila kuangalia mwili wake. Mapendo roho yanaanza mbele katika nyumba, na yanaonekana katik vitendo vyetu vya kila siku; hayawezi kubadilika katika furaha wala katika mateso.

Basi, wababa na wamama, Mungu mwenyewe ni mapendo. Kama sisi ni mapendo sawa naye Mungu ni mapendo, dunia itaku na amani.

Kwa kuyaweza mapendo haya ya roho, ni lazima tuanze kuu saidia mwili tunauona kwa macho. Kwa mfano: kumpa mtu c kula, kumpatia fasi ya kulala, kumtunzisha akiwa mgonjw kuwasaidia maskini, hata kuwasaidia watu kwa kupata kaz ao masomo, na vivi hivi. Tukitendeana vile, sherti tuta pata kuwazaa watu ku roho.

## <u>Mawazo ya Mungu (Utatu Mtakatifu).</u>

Mungu ni Jamaa tangu milele, kwani ni Baba, Mwana na Ro Mtakatifu. Mapendo ya Umoja. Nafsi yote tatu si miungu mitatu, ila ni Mungu mmoja, kamili, asiyegawanyika.

Baba ni Baba wa Mwana milele; Mwana ni Mwana wa Baba mi lele; na Roho Mtakatifu ni nguvu ya mapendo ya Baba na Mwana, anawaunganisha milele.

Mungu ni roho tupu ao Mawazo; mtu anafanana naye kwa ro naye pia ni baba, mwana, na ana roho ya umoja kwa wengi kama Yeye mwenyewe.

a) <u>Mawazo ya Ubaba.</u>

Baba ni mwenyi kuleta, kuchunga na kukomesha uzima. Mun Baba analeta uzima katika kuumba, anachunga na kukomesh uzima katika huruma yake isiyo na mwisho; japo waana wa wanaishi daima katika ukosefu, anawahurumia tu, wakiwa wangali hapa duniani.

Mtu ni mwili na roho; basi anao ubaba ao umama wa mwili akizaa watoto duniani, kuwachunga na kuwakomesha.

Mungu aliwaambia Adamu na Eva: "Nendeni, mkajaze dunia." Mtu akiwachunga vema watoto wake, anachunga mapenzi ya Mungu na amri zake.

Ubaba ao umama wa roho, ndio ubaba ao umama wa kimungu. Mtu ni baba wa kweli akileta, kuchunga na kukomesha mtu mwenzake karibu na Mungu, ili apokee ndani mwake uzima wa Mungu : kumzaa katika uzima wa Mungu bila kuangalia ukosefu wa wengine, akiwa na huruma tele kama vile Mungu mwenyewe. Sala ya'Baba yetu' inatufundisha tuwe na huruma kwa wengine ili tustahili kuhurumiwa na Mungu.

b) <u>Mawazo ya Umwana.</u>

Mwana ni mwenyi kupokea uzima kwa Baba, na kuuchunga vema. Mungu Mwana anajinyenyekea na kujishusha na kujifanya mtu kusudi ya kutimiza mapenzi ya Baba yake. Anajishusha hata kuwa mwana wa mtu, akipokea kwa mama uzima wa mtu, kuuchunga na kuukomesha. Kumbe Mwana ni mwenyi kujishusha. Kama vile mtu ni mwili na roho, umwana wa mwili huonekana ukipokea uzima kwa wazazi, kuulinda na kuukomesha katika utii, upole, unyenyekevu ...; amri ya ine inatufundisha mapashwa ya watoto kwa wazazi wao.

Umwana wa roho ni katika utii: katika kutii na kutimiza mapenzi ya Mungu kwanza, pia na ya Eklezya, mama yetu. Mwana wa mtu ni pia mwana wa Mungu; kumbe ni afazali kujishusha kwa mtu mwenzako katika utii, upole, unyenyekevu, utulivu, na mapendo yote.

c) <u>Mawazo ya Roho Mtakatifu.</u>

Roho Mtakatifu ni mwenyi kuunganisha, kupatanisha. Ile iliyotengana, anaunganisha kuwa moja. Mungu Roho Mtakatifu ni Mapendo anayeunganisha Baba na Mwana, na nafsi yote tatu ni mpaka Mungu mmoja. Hata Mwana akashuka duniani kwa nguvu yake Roho Mtakatifu.

Ni sawa katika mtu : Roho Mtakatifu ni mwenyi kazi ya kuunganisha mwili na roho ya mtu, yapate kuwa moja mbele ya Mungu. Na katika ndoa, mapendo ya bwana na bibi yanaonekana ikiwa kila mmoja anabaki mwaminifu kwa agano yao ya ndoa.

Mapendo ya kuungana katika roho huonekana katika kuungana na Mungu katika mawazo yake makubwa, na pia katika kuungana na Eklezya tukitii mapenzi yake yote. Roho Mtakatifu anawaunganisha watu wote wawe mmoja rohoni mwao katika mapendo.

Umoja huu tunaupata katika sakramenta, na sala, na ibada, tukiwatumikia wenzetu na unyenyekevu, na upole, katika utii, na masikilizano, na masaidiano.
Mawazo haya yote huanzia kutimizwa nyumbani, katika jamaa kati ya bwana na bibi, kwani wao ndio msinji wa jamaa zot duniani.

Wababa na wamama, hivi Mungu yupo Baba, Mwana na Mapendo, sisi vilevile tupo na mawazo haya yote. Tupo baba ao mama tukikumbuka watoto; tupo mwana tukikumbuka wazazi; tupo bwana tukikumbuka bibi; tupo bibi tukikumbuka bwana. Ndio Utatu Mtakatifu kati yetu. Tunaweza pia kuzungumza juu ya Utatu Mtakatifu kati ya baba na mama, hata kati ya wale wasio na watoto wa mwili katika ndoa yao,

- Baba awe baba wa mke wake,
  mwana wa mke wake,
  na bwana wake.
- Mama awe mama wa mume wake,
  mwana wa mume wake,
  na bibi yake.

Wazaane na waungane kati yao, wapate uzima, uzazi na mapendo ya umoja. Waonyeshe pia vile mapendo ua ubaba ao umama, ya umwana na ya umoja yanayotuunganisha na Mungu Baba anayetupatia roho ya umwana; yanayotuunganisha pia n Mungu Mwana anayetupatia roho ya umwana; yanayotuunganish pia na Roho Mtakatifu anayetupatia roho ya kuungana katik umoja.
Vilevile kwa Padri, Frera ao Bikira, ni baba ao mama pamoja na Mungu Baba akikumbuka waana wake wa roho anaowapati uzima wa Mungu; ni mwana pamoja na Kristu akizaliwa kwa Mungu na kwa mtu na akijinyenyekesha apate kuikomboa dunia ni mapendo pamoja na Roho wa Mungu akiunganisha watu na Mungu, tena mtu na mtu mwengine.

## 9/ ALAMA YA MSALABA.

Alama ya msalaba inatukumbusha Utatu Mtakatifu katika sif yake. Tunapofanya alama ya msalaba, tupo tunaomba Mungu atupatie yale mawazo yake tatu.
Ni hapo tunasema hivi: "Vile upo Baba, na mimi niwe baba wa huruma; vile upo Mwana, na mimi niwe mwana kwa kuzaliw vile upo Roho Mtakatifu, na mimi niwe roho mapendo ya umo ja.

Kumbe, wababa na wamama, wakati tunapofanya alama ya msalaba, tuifanye vema na heshima, tukikumbuka tunafanya nini. Tusiifanye mbiombio, pasipo hata kuwaza... Mnasikia kuwa baba sawa na Mungu, mwana na roho mapendo ni kitu cha ajabu sana.

## 10/ HESHIMA MU NYUMBA YA MUNGU.

Heshima na unyenyekevu nyumbani mwa Mungu!

- Mbele ya kuingia nyumbani mwa Mungu. Hatuwezi kuingia kama vile mu "bar". Tunapofika mlangoni, tunafanya alama ya msalaba na maji ya baraka, ao pasipo maji ya baraka, na tunasema : "Wewe Mtakatifu (Yosefu, ao Andrea, ao vivi hivi), Msimamizi wa nyumba hii, nakutolea mawazo yangu, upate kuyapeleka mbele ya Mungu wetu."
- Kupiga magoti. Tunapiga magoti tukasema: "Mungu wangu, mwili wangu ni udongo na utarudia kwa udongo; roho yangu iko mikononi mwako; siku ya kuachana na mwili, ipate kufurahi nawe katika sifa yako milele."

Kiisha tunaenda pa fasi yenyi kuwa wazi kwa kuongeza sala zetu.

Ni vile, wababa na wamama, tunavyoona katika dunia, tukitaka kuonana na kuzungumza na mfalme : tunapashwa kupita kwa mtumishi wake, na yule atatupeleka kwa bwana ao mfalme: tunapashwa kuwa na unyenyekevu mbele yake Mungu kupita mbele ya wafalme wa dunia.

=§=§=§=§=§=§=§=§=§=§=

## I.- MUNGU NA BIKIRA MARIA.

Tangu milele, mbingu na dunia havijaumbwa bado, Mungu alikuwako : Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu Mapendo ya umoja ndani mwake.

Mungu wa mapendo yote akawaza katika Ubaba wake alete uzima wake wote kwa kiumbe kimoja alichokipendelea zaidi; katika Umwana wake akawaza azaliwe kwa kiumbe kile, hata kubaki mwana wake milele; katika Mapendo yake ya umoja, akawaza aungane naye, mu vyote, hata katika umungu wake. Kiumbe kile ambacho kiliteuliwa na Mungu tangu milele, dunia na mbingu havijakuwako bado, katika mawazo yake, ndiye Bwana Yesu, nafsi ya pili ya Utatu Mtakatifu.

Basi, Bwana Yesu ndiye mtu wa kwanza katika mawazo ya Mu gu. Na hata kama watu wote wako katika mawazo ya Mungu tangu milele, lakini Bikira Maria aliwaziwa na kuchagul na Mungu kuliko watu wote, saa ileile Mungu alipowaza k tuma Mkombozi duniani. Naye Bikira Maria ni kweli "jama yake Mungu: kwani ni mwana wake, maana ameumbwa naye; n mama yake, kwa sababu Mungu mwenyewe amejishusha hata k kamata mwili kwake (Luka 1, 31-32); ni mapendo kwake, k sababu ameungana na Roho Mtakatifu. Ni kwa umoja huu Mw akajifanya mtu ndani mwake, akikamata mwili kwake.

Bikira Maria alikuwa katika mawazo ya Mungu saa ile Mun alipowaza kuumba vitu vyote, hata vyote ni kwa furaha y kwani Mungu alijua ya kama Bikira Maria atakuwa duniani Mama wa Mwana wake.

Ni pale Bikira Maria anasifiwa kuliko watu wote na wama wote, kwani alijazwa na Utatu Mtakatifu; ni kwake kwanz tunajulia kama Mungu ni Baba, Mwana, na Mapendo ya Umoj Ikiwa Mungu Mwenyezi wa vyote amejishusha na kujitolea mawazo yake yote kwa mwanamke, tangu milele, katika maw yake, hata kukamata mwili kwake, basi mtu, aliye sura mfano wa Mungu, atafanyaje kwa yule mbarikiwa kuliko wa wake wote? Na atafanyaje kwa yule mke wake, bibi yake, aliye sura na mfano wazi wa yule mama wa Mungu?

Kwa nini basi kumheshimu Maria na kumtaja Mama, Malkia wetu, na vivi hivi, kama nyumbani mwetu, mke aliye sura mfano wazi wa Maria, anazarauliwa na kutajwa mtumwa? Mk wetu, ndiye aliyekuwa wa kwanza katika mawazo yetu, ana hili basi heshima yote; na ni katika kujitolea mu vyote mmoja kwa mwengine, tutatimiza mawazo ya Mungu na Maria nyumbani mwetu.

## II.- MALAIKA :

a) Hali yao.

Pamoja na kuumba mtu, Mungu akaumba viumbe vingine visivyo na mwili, ndio wamalaika wenyi nguvu na akili t Akawaumba wengi sana, wenyi kuachana kwa akili na kwa d ja mbalimbali. Kati yao, akamwumba mmoja akimpa akili n nguvu na uzuri mkubwa mno: ndiye Lucifer, maana yake "m nyi mwanga mkubwa", wa akili na elimu tele.

b) Kujaribiwa kwao.

Kama vile kwa watu, Mungu aliwatakia uzima wote, uzazi na mapendo yote, kama yeye mwenyewe; ndipo akawaomba wampende pia kiumbe chake mtu. Wakitimiza mapendo hayo, atawapokelea kwake na kuishi pamoja nao katika uzima wa milele... Malaika wengine wakakubali amri hiyo ya Mungu, wakiongozwana Malaika Mkuu Mikaeli. (Jina Mikaeli, maana yake: "Ni nani atakayebishana na Mungu?")
Wengine lakini wakiongozwa na Lucifer wakakataa kupendana kati yao, wakijivunia uzuri wao na kujenga mipaka na uchaguzi; walikataa pia kumpenda mtu, wakakataa kabisa kutii na kujinyenyekesha mbele ya Kristu, Mungu-mtu.
Ndipo wakawa makundi mawili: kundi moja la wenyi kuwa na mapendo kwa Mungu na kati yao, na kwa mtu pia; na kundi lingine la wenyi kukataa mapendo yoyote.

c) Malipizi yao.

Lucifer na wote waliokubali mawazo yake wakabaki katika upekee wa milele bila mapendo, lakini na akili yao yote, na nguvu yao yote; ndiyo Jehanama. Ndipo Lucifer akageuka kuwa Shetani, Mlozi, Mwenyi kuua uzima anapoukuta. Ndani mwake si baba, si mwana, si mapendo. Anajazwa na chuki na hasira, ndio uharibifu wote.
Kwa wale waliokubali mapendo lakini, Mungu akaleta uzima wa milele mbinguni.

d) Shauri.

Mtu ni mlinzi wa mwili, alipewa wa kwanza amri hiyo ya mapendo kwa Mungu na kwa jirani yake, mbele ya kupata uzima wa milele mbinguni (cf. Deut.6,5; Lev.19,18; Lk.10,27; Mt.22,36-40; Mk 12,28-31; Yo.13,34). Lakini tukiangalia nyumbani mwetu na nje pia, tunafuata zaidi mawazo ya Lucifer, kuliko mawazo ya malaika wema.
Katika vitendo na mifano yetu, hasa tukipata bahati ya kuwa na cheo pa kazi, ao kujua mengi, tunajivunia tu ukubwa wa elimu yetu, na uzuri wa mwili, na tunawazarau wengine. Hii inazaa mipaka, ukabila, chuki na lufu!
Kumbe kwa kupata uzima wa milele kwa Mungu, tufuate mawazo ya malaika wema: tupendane nyumbani kwa mawazo yetu yote, bila kuangalia uzuri wa nje. Tupende pia watu wengine kama vile twajipenda kwa mawazo yote, ndiyo kusema, kuwatendea matendo yenyi kuamsha ndani mwao mawazo ya mapendo kwa Mungu na kwa watu wengine; ndiyo namna ya kustahili kuitwa waana wa Mungu.

N.B. Malaika walinzi ni wamoja wa wale waliokubali mawaz
ya Mungu: mawazo ya mapendo kwa Mungu, kwa malaika wenzao, na kwa mtu. Ndivyo basi, na sisi tuwe walinzi wa mawazo ya mapendo kati yetu, baba kwa mama, mama kwa bal na ndugu kwa ndugu. Pale tutakuwa ku ngambo ya Mikaeli tukimtii Mungu na tukipigana na giza za Lucifer.

## III.- MAFUNDISHO YA ADAMU NA EVA.

a) Mungu anawaumba. (Mw. 1,..- 3,..)

Mungu alipokwisha kuumba mbingu na dunia, na viumbe vyote vyenyi kuonekana na visivyoonekana, vyote vilipokw sha kuwa tayari, akasema: "Tuumbe mtu, kwa sura na mfan wetu, awe mkubwa wa viumbe vyote, atawale dunia." Hapo Mungu akatwaa udongo, akaufinyanga kuwa sura ya mtu mwan ume, halafu akatiamo mawazo yake yote tatu, na mara mtu mzima akasimama na akaitwa Adamu, maana yake : aliyetoka kwa udongo. Mungu akamtia katika bustani ya anasa, para zo ya dunia, na mtu akawa na kazi ya kuvipa viumbe ving majina. Mtu alikuwa mwenyi heri na furaha tele kwa ajili ya vyote alivyopewa na Mungu. Lakini alijiona kuwa katil upekee, sababu viumbe vingine vyote vilikuwa viwili viw na yeye hakuwa na ule aliyefanana naye.

Mungu alipotambua mawazo yake, akasema: "Mtu huyu, si v awe peke yake; nitampa mwenzake atakayeungana naye, kus diana na kupendana naye katika mawazo yote." Hapo, Bwan Mungu akamtia Adamu katika usingizi, na kiisha akamtosh ubavu wake mmoja akaumba nao mwili wa Eva, na akamtolea Adamu; na Adamu akampokea, akafurahi na kusema: "Kweli, huyu niliyekuwa naye katika mawazo yangu. Tangu leo nit ungana naye, nitasaidiana naye katika mawazo yote tatu. Na akampa jina lake Eva, maana yake 'mama wa wazima'. (Hapa tunatia mifano ya vile bibi na bwana wanavyoona).

Mungu aliwaambia Adamu na Eva: "Muwe siku zote pamoja, msaidiane. Tangu sasa, mwili huyu si wako tena peke yak Adamu; ni pia wa Eva, mke wako. Na wewe Eva, mwili huyu wako peke yako, ni pia wa Adamu. Msijikatalie kitu. Vyo mwifanye mpaka na masikilizano makubwa kati yenu. Muwe kimoja kati yenu na mimi Mungu, Bwana wenu, katika masi lizano, masaidiano na umoja wa mapendo ya kweli. Ni hiv nitakuwa siku zote kati yenu, na kiisha nitawachukua ka paradizo ya mbingu, kwenyi furaha ya milele. Mfurahi na te, lakini msile matunda ya mti wa wema na wa ubaya. Mk matunda hayo, mtakufa."

b) Kosa la Adamu na Eva. (Mw. 3,1-19)

Adamu na Eva walibaki wenyi heri na furaha, kama v
Mungu alivyowatakia.
Lakini siku moja, Eva alimwacha Adamu na akaenda kutem
peke ndani ya bustani. Na huko akashawishiwa na shetan
aliyejificha ndani ya nyoka. Shetani akamwuliza Eva: "
babu gani mnakatazwa kula matunda ya miti yote iliyo k
tika bustani?" Eva akajibu: "Tunakula matunda ya miti
isipokuwa yake ya mti mmoja wa wema na wa ubaya. Tukil
tunda lake, tutakufa." Shetani akasema tena: Sivyo, mk
tunda la mti ule, hamtakufa, lakini mtakuwa na akili n
gi, na mtatenda yote sawa na Mungu."

Basi Eva akashindwa na kishawishi, akatwaa tunda l
mti ule, na akala. Hapo akajiona kama anamkosea Mungu,
shetani akamkimbia.

Eva akarudi kwa Adamu, naye Adamu alimtambua kama
kwisha kukosa na amekula tunda walilokatazwa. Na Eva a
mwambia Adamu kama "Ni Shetani aliyenidanganya." Halaf
Eva akampa naye Adamu sehemu ya tunda alilomletea. Ada
akala, naye akamkosea Mungu. Wote wawili walipokwisha
kosa, wakajiona utupu, na wakakimbia, wakaenda kujific
Kiisha wakasikia sauti ya Mungu ikiwaita na kumwuliza
mu: "Sababu gani unajificha?" Adamu akajibu: "Ni Eva a
nikosesha." Na Eva naye akasema: "Ni shetani aliyenida
nya." Na pale Mungu akawapa malipizi, wote watatu.

Kwa Adamu, Mungu akasema: "Kwa sababu uliitika sau
ya Eva, tangu leo naapisha udongo, na utapata chakula
ko kwa kazi na jasho la uso wako."

Kwa Eva, Mungu akasema: "Kwa kuwa uliitika sauti y
shetani, utabaki chini ya bwana, na utapata mateso kat
uzazi wako."

Kwa shetani, Mungu akasema: Kwa kuwa umedanganya E
nakuapiza: tangu leo utatembea katika udongo, na pua y
itanusa uvumbi. Na pia natia adui kati ya kizazi chakc
kizazi chake Eva, nacho kitakuvunja kichwa."

Halafu Mungu akawafukuza Adamu na Eva katika busta
ya anasa. Kule walikokwenda, wakaanza kusikitika na ku
lia. Na Mungu akawaelezea kama: "Nitawahurumia na nita
tumia Mkombozi, na huyu atazaliwa na bikira mmoja asiy
bwana."

N.B. Katika mafundisho ya Adamu na Eva, tunafasiria hi
tunaonyesha ubaya wa zambi katika upekee juu ya a
ya sita.

Tunafundisha pia juu ya huruma mbele ya makosa ya mwenzetu : njia ya kweli si kuachana, lakini kushauriana na kuhurumiana.

) Mashauri na vizila.

Katika mashauri haya, wababa na wamama, inakatazwa kujiangalia ku mwili wetu wa ubaba ao wa umama na kujikamata na kucheza nao. Tukitenda vile, ni hatari ya kuangusha maji yetu ya uzima chini, na itatusukuma pia kwa usharati.

Tukiepuka hiyo yote, itatusaidia kuchunga vema ndoa yetu.

Basi,wababa na wamama, tumekwisha kusikia mafundisho ya kosa la Adamu na Eva, na ndani ya mafundisho yale tunakutamo: - Kiburi: mtu mwenyi kuburi tunaona kila mara kama hawezi kusikilizana na wengine.

- Majivuno: inaonekana kila mara kwa watu wanaojiona kuwa bora kuliko wengine.

- Upekee: katika upekee, kila mara tunaingia katika lufu. Mnaona kama Eva,alipotaka kubishana na shetani katika upekee, alishindwa na kuanguka katika zambi. Kama angeenda kumwelezea Adamu mbele, na wangekuwa wote wawili, wangemshinda shetani.

- Utii: ndani ya nyumba, kwa wakubwa ao kwa wadogo na kati ya wenzetu, tunapashwa kila mara kuwa na utii, kwani pasipo utii, hakuna masikilizano wala maendeleo ndani ya nyumba, katika kundi na popote.

## IV.- KAINI NA ABEL : WATOTO WA ADAMU NA EVA.

Kiisha kufukuzwa katika bustani ya anasa, Adamu na Eva walienda kuzaa watoto wawili : Kaini na Abel.

Kaini alikuwa mlimaji, na mdogo wake Abel alikuwa mchungaji. Kaini alikuwa mwenyi kiburi sana na majivuno, na Abel alikuwa mwema na mtii.

Wote wawili walizoea kila mara kumtolea Mungu sadaka zao. Kaini alikuwa anatolea mavuno ya mashamba yake, na Abel yeye alimtolea Mungu wanyama aliokuwa akichunga. Sadaka ya Abel lakini ilimpendeza Mungu, kwani alimtolea hiyo na roho ya mapendo, tena alichagua nyama wazuri na wanono, kati ya nyama zake zote.

Kaini alipoona kama sadaka ya Abel ilimpendeza Mungu kuliko zake, akamwonea ndugu yake wivu ...

na mawazo ya kumwua yakamfikia; hata siku moja, wakienda kutembea pamoja, Kaini akamrukia Abel na kumwua. Kiisha Kaini akaenda kujificha. Lakini Mungu aliona vyote na akamwuliza Kaini: "Ndugu yako yupo wapi?" Kaini akajibu: "Sijui; mimi si mchungaji wa ndugu yangu." Mungu akamwambia: "Damu ya ndugu yako inanililia toka dunia; sasa utafukuzwa katika udongo huu. Ukiulima, hautakuzalia matunda, na utatangatanga duniani kote." Hata wazazi wao, walipopata habari hii ya uchungu, wakamfukuza Kaini.

Kumbe, wababa na wamama, mnaona kama kosa lile la kwanza la Adamu na Eva linazidi kuendelea hata kwa watoto wao. Basi tukitolea sadaka yetu kwa Mungu na kwa jirani, inafaa tuitolee na roho nzuri yenyi mapendo, ili iwe sadaka ya kweli, ya kufanana na ile ya Abel.

Roho ile ya Kaini inaonekana kila mara, humu duniani: mtu mbaya anapoona mwenzake anayefuata vema njia ya Mungu, anayetumika vizuri kazi yake na anayechunga vizuri nyumba yake na kuonyesha mifano na vitendo vizuri, mtu mbaya atamchukia, hata kutaka kumwua, pahali pa kupima naye kufuata na kutenda matendo yake mema.

## V.- KUZALIWA KWA BIKIRA MARIA NA KUKOMEA KWAKE.

Katika kizazi cha Daudi, kulikuwa mtu mmoja mwema, jina lake Yoakimu, na mke wake Ana. Yoakimu na Ana walibaki siku nyingi sana katika ndoa yao, pasipo kumzaa mtoto. Walisikitika sana muda wa maisha yao, sababu hawakukuwa na mtoto. Lakini hawakukata tamaa, walimtumaini tu Mungu siku zote. Siku moja Ana akajiona kama ana mimba. Wote wawili, hata watu wengine, walisitasita, waliwaza tu kama anapata ugonjwa. Mimba ile iliendelea na kukomea. Wakati ulipotimia, akamzaa mtoto mke mzuri sana, mpole na mfurahivu sana. Wazazi wake wakampa jina lake 'Myriam'.

Kumbe, wababa na wamama, kama tukibaki siku nyingi katika ndoa yetu pasipo kupata watoto, tusikate tamaa, lakini tumtumaini tu Mungu peke yake, kwani vyote vyatoka kwake.

Bikira Maria alikomea na tabia nzuri; alikuwa mtoto mwema, mfurahivu, mwenyi mapendo, mtii, na mwenyi masikilizano. Katika kukomea kwake, Bikira Maria aliachana na watoto wengine katika vitendo na mifano yake.

Muda wa kukomea kwake, Bikira Maria hakutenda zambi hata mara moja, hata ya kuwaza. Hakuwa na vishawishi vya zambi hata mara moja, kwani alikingiwa na Mungu tangu milele.
Wazazi wake Maria walimwelezea kila siku neno la Mungu; na Bikira Maria alipenda sana kusikiliza na utii neno la Mungu wake. Kila siku Bikira Maria alikuwa anasali akisema: "Mungu, tuma Mkombozi yule uliyemwagana na makambo wetu wa kwanza, kwani dunia inaharibika."
Katika ujana wake, Bikira Maria alikaa katika hema la mabikira; mule alijitolea kwa kazi ya kuchunga nyumba ya Mungu, na katika sala. Halafu, wenzake walipoona vile, wakamchukia.
Basi, wababa na wamama, sisi wazazi tusijiwazie ya kama ni sisi peke yetu tu tunajua Mungu, lakini tuwasaidie watoto wetu katika maelezo na mifano, nao waweze kupata vilevile kumjua Mungu sawa na sisi. Tuwafundishe kusali, kusikiliza misa, na tuwafasirie mambo ya Enjili. Tuwajulishe sanamu ya Bwana Yesu na ya Bikira Maria, ili kote watakakoenda, waitambue bila shaka. Tuwawezeshe kuwa wema, watii, wapole, wanyenyekevu, ili wao pia wapende jamaa hii ya Mungu.
Kwa sisi, wamama, tunasikia kazi aliyofanya Bikira Maria nyumbani mwa Mungu; hata mnaona mabikira wetu wa sasa wanaoshinda mchana kutwa kanisani tu kwa kutengeneza na kutayarisha vyote na kuonyesha heshima yao kwa Bwana Mungu. Kumbe kazi ile ya Bikira Maria na ya mabikira wetu ni pia kazi yetu ya kuchunga vema nyumba yetu, kuifanya safi, ipendeze bwana na watoto; ni vema pia kusaidia kazi ya nyumba ya Mungu: kukolopa, kupamba nyumba ya Mungu, kutosha uvumbi ku mbao za kanisani.

## VI.- BIKIRA MARIA ANACHUMBIWA NA YOSEFU MTAKATIFU.

Wakati ule, Bikira Maria alirudi kwa wazazi. Lakini katika mawazo yake, hakukuwa na tamaa ya kuolewa.
Katika kizazi kila cha Daudi, kulikuwa mtu mmoja mwema, jina lake Yosefu, aliyebaki pasipo kuoa, sababu alitafuta mke mwema na mwenyi kumcha Mungu kama yeye. Katika kutafuta kwake, alipata habari ya kama kuna kijana mmoja mwanamke, jina lake Maria, mwenyi tabia nzuri sana kama vile alivyotaka.

Halafu Yosefu akaenda kwa wazazi wa binti yule, akapatana nao, na akapatana pia na binti mwenyewe. Wote wawili wakasikilizana, na Yosefu akatoa mali. Sasa wote wawili walibaki na kitumaini, na kusali, wakingojea siku ya ndoa yao, kama vile ilivyokuwa desturi ya Mayahudi.

## VII.- MAFUNDISHO YA YOHANE MPENZI WA YESU.

(Yo.21,20)

Tunajua kama Bwana Yesu alikuwa na mitume kumi na wawili; na kati yao kulikuwa mtume mmoja mdogo kuliko wote aliyekuwa mtii, mnyenyekevu na mwenyi mapendo tele. Ndiye Yoane mtume. Kwa ajili ya hali ile ya Yoane, Mungu Roho Mtakatifu alimwangazia fumbo la umoja wa Bwana Yesu na Bikira Maria.

Hapo, siku moja, Yoane alijiuliza juu ya Bwana Yesu na Bikira Maria ya kama: "Mapendano yao yanapita yale ya mama na mtoto wake, na umoja wao unapita ule wa bibi na bwana! Kweli sijaona bado mama na mwana wake wanaopendana vile; siwezi kusikia namna ya umoja na ya mapendo yao!" Kiisha kuwaza vile, Yoane alikumbuka na kusema: "Nawaza juu ya Bwana Yesu hivi kama Yeye ni mtu wa dunia; lakini 'yeye anayesadiki kama Yesu ni mwana wa Mungu' (I Yo.5,5) anaweza kusikia mambo yanayopita mawazo ya dunia. Kumbe nilikuwa nasahau kama Yeye Bwana Yesu alizaliwa si kwa damu, wala kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, lakini kwa Mungu (Yo.1,13) Ni kweli ninakosa sana; sasa nitafanya nini? Kwa kuwa yeye pia amekwisha kuja mawazo yangu yote. Kumbe niende tu nikatubu na kumwomba huruma. Nimwambie tena kama mimi namsadiki: "Ndiwe Kristu, Mwana wa Mungu aliye mzima.(Mt.16,16)"

Yoane akaenda kwa Bwana Yesu akamwelezea mawazo yake yote vile alivyojiuliza juu yake. Bwana Yesu akamjibu na kusema: "Heri kwako, Yoane, si kwa nguvu yako, mwanangu, umevumbua ile yote, ila Roho Mtakatifu alikuangazia upate kujua fumbo hili la umoja wetu na Mama yangu. Tangu leo, ukitaka, itatendeka kwako pia, na utakuwa katika umoja wetu. Bikira Maria atakuwa Mama yako kama vile ni Mama yangu kwa nguvu ya Roho Mtakatifu (Lk 1,35); nawe utakuwa mwana wake kama vile mimi niko mwana wake. Utakuwa naye katika umoja na mapendo kama vile mimi niko naye." Na kiisha kufa kwake Bwana Yesu, Yoane alimchukua Mama Bikira Maria nyumbani kwake (cf Yo.19,25) .

Yoane alifurahi sana akajazwa na Roho Mtakatifu, maana yeye alimjua Bwana Yesu na Bikira Maria.

- Wababa na wamama, mafundisho ya Yoane mtakatifu ya tufundisha na kutufungulia njia ya Mungu. Yoane alikuwa mtii mbele ya Mungu na ya watu. Hakukuwa na majivuno wa na tamaa mbaya, ila na mapendo tu.

- Alipokwisha kujiuliza juu ya Bwana Yesu, hakusita kwenda kumpasha yote Bwana Yesu. Bwana Yesu alimhurumia na kumwingiza kabisa katika jamaa ya umoja wa roho. Kuungama kwa Yoane kunatufundisha sisi wote ya kama: tunapokosa, tusikawie, lakini twende upesi kwa Bwana Yesu kuungama makosa yetu. Tusiogope kuomba huruma, hata nyumbani mwetu ao kwa mtu mwengine.
Kumbe, wababa na wamama, tukitubu makosa yetu kwa watu wenzetu na kwa Mungu, na roho ya unyenyekevu, kiisha twende kuungama kwa Padri, tutapata maondoleo na kuingizwa katika Jamaa ya Ufalme wa Mungu na kurudishiwa Uzima wa Baba wa mbingu.

## VIII.- KUZALIWA KWA MARIA MADELEINE KATIKA JAMAA YA BWANA YESU NA MITUME.

Bwana Yesu alifundisha popote katika miji ya Palesti (Lk 8.1). Mafundisho yake yalivumwa na kusikilika sana; watu walikuwa wanasema: "Huyu alikuja kueleza habari nje sana, habari ya mapendo, tupate kupendana kwa kuwa umoja wa kweli."

Siku moja, Bwana Yesu alifika kufundisha katika mji mmoja uitwao Magdala. Na katika mji ule, kulikuwa mwanamke mmoja, jina lake Maria wa Magdala; mwanamke yule alikuwa ndumba mwenyi sura nzuri na mwenyi kujipamba sana, kama vile tunavyoona zoezo la ndumba wote. Naye aliposikia kama Bwana Yesu anakuja kwa kufundisha katika mji wao, akaenda kuyasikiliza mafundisho yale ya mapendo kwa Bwana Yesu. Ni kweli Bwana Yesu alikuwa anafundisha mapendo na umoja wa kweli kati ya watu; lakini Maria Madeleine alisikia mafundisho hayo kwa namna yake, na alipatwa na tamaa kubwa sana, na alisema moyoni mwake: "Kijana huyu mzuri hivi na mwenyi kufundisha mafundisho ya mapendo anatoka wapi? Kumbe wakati atakapokwisha kufundisha, nitamfuata ili anifundishe nami mafundisho haya. Huku kwetu, ni mimi peke najua mapendo; kumbe na yeye vilevile anajua mapend

kunishinda mimi? Nitamfuata tu, nikaone mapendo yake."

Basi Bwana Yesu alipokwisha kufundisha, watu wote walisambaa; lakini Maria wa Magdala akamfuata Yesu, akamwambia: "Bwana, nilisikia mafundisho yako yote na yalinipendeza sana kwa sababu ulizidi kufundisha mapendo, mtu na mtu wapendane." Bwana Yesu akamjibu: "Ndiyo sababu mimi nilitumwa duniani: kwa kuwafundisha watu wapate kujua mapendo." Lakini Bwana Yesu aliona ndani ya roho yake muko tamaa ya usharati; kwani Maria Madeleine hakujua kama huy ni Mungu. Bwana Yesu lakini hakumfukuza, bali aliendelea kuzungumza naye ili apate kumgeuza, aache mapendo yake ya mwili na apate kuwa na mapendo ya kweli ya Mungu. Kwa hiy Bwana Yesu hakumficha kitu, ila alimwelezea waziwazi kama "Wewe hauna mapendo ya kweli ndani yako. Kati ya wale wot uliotembea nao, ni nani unayempenda zaidi? Umekwisha kueneza wanaume wengi, na wale wote uliokwisha kutembea nao, ungali unawapenda tena? Umekwisha pia kuvunja ndoa ya wengi, hiyo ni mapendo ya kweli?"

Maria Madeleine aliposikia hayo yote, aliogopa akatak kukimbia, kwa sababu aliona kama huyu si mtu sawa na watu wote. Bwana Yesu akamwelezea: "Usikimbie Maria, wala usishangae; mimi nakujua wewe wote mzima, najua pia mawazo yako na pia vitendo vyako vyote. Hausikii kama niko Masih Nilikuumba, niko Mungu na Mkombozi wako. Sasa nitakufundisha mapendo ni kitu gani sababu mimi najua mapendo. Ungeniomba, ningekuelezea vizuri."

Maria Madeleine akamjibu: "Bwana, ni kweli, najua sas kama upo nani. Nami natubu zambi zangu zote, sitafanya te na undumba. Nakuomba sana unipatie nami mapendo yale, nit jitolea mimi wote kwako, nitakuwa wako, sitarudi tena kwa mtu hata mmoja, kwa sababu naona maisha yale niliyokuwa nayo ni ya uharibifu." Japo alisema hayo yote, Maria Madeleine hajafumbua bado umungu wa Bwana Yesu. Na Bwana Yesu akamwambia: "Mimi sitakuelezea kitu tena; lakini ukitaka kunifahamu zaidi na kutambua mapendo ni nini, basi nenda kwa Mama yangu Maria. Yeye ataweza kukufundisha mapend ni nini, kwa sababu ni kwake Mungu alitaka kujitolea wote mzima (Lk 1,31-33,35), na kwa hiyo ni yeye mmoja tu mweny heri katika wanawake wote (Lk 1,42)." Maria Magdala akamwuliza: "Mama yule mwenyi heri yupo wapi?" Yesu akajibu: "Uende pa Nazareth, utampata."

Kwa kuwa Maria Madeleine alikuwa na tamaa kubwa ya kuwa na Bwana Yesu, aliendа mbio kwa Bikira Maria, akamwomba na kumweleze a yote ili ampe Mwana wake, awe naye katika umoja na mapendo ya lote. Bikira Maria alimpokea Maria Madeleine na alimwuliza: "Utamwamini na kukubali kuongozwa naye kama ni Mungu Mkombozi?" Maria Madeleine akaitika yote. Halafu Bikira Maria akamfundisha namna ya kuwa na umoja na Bwana Yesu, akisema: "Kwa kuwa umoja naye, unapashwa kumheshimu, kumtumikia na kumfuata popote. Ni vile mimi namwamini, namtumikia na kumfuata popote katika mapendo matakatifu. Lakini ujue kama ni Mkombozi wa watu wote; atateswa na kiisha atakufa kwa ajili ya wote: ndiyo njia yake ya kufika kwa ufufuko." Bikira Maria akamfundisha Maria Madeleine namna yote ili Maria Madeleine ageuke na kuwa katika Jamaa ya kweli ya Mungu. Alipokwisha kumsikilizisha hayo yote, Maria Madeleine alirudi kwa Bwana Yesu na kumpasha yote. Bwana Yesu akamjibu: "Najua yote, najua mawazo ya roho yako. Sababu gani haukuweza kufahamu usemi wangu? (Yo.8,43)... Nani kati yenu ataweza kunishtaki juu ya zambi? ...yeye aliye wa Mungu anasikia maneno ya Mungu; basi nyinyi hamsikii kwa sababu nyinyi si wa Mungu (Yo.8,46-47) Uende kwako, usali, Mungu akuangazie: 'kilichozaliwa na mwili, ni mwili'(Yo.3,6), na 'mwili haufai kitu'(Yo.6,63). Maria wee! mimi nilikuja duniani kwa kuwafundisha watu mapendo yenyi kuitwa Mungu (I Yo.4,9), na wewe usipozaliwa na Roho, hautaweza kusikia mawazo ya roho."

Japo alielezwa peupe ya kama "huyu ni Mkombozi", Maria Magdalena hakufunguka upesi; alibaki na tamaa ile ya kimuntu. Basi alikwenda kwake na kitumaini kikubwa, akajitayarisha namna yote kama vile mnavyojua zoezo la ndumba. Akachunga weee, hakumwona Bwana Yesu. Halafu, alipochoka, ...katika mawazo yake aliangaziwa na Roho Mtakatifu, akatambua umungu wa Bwana Yesu. Aliposhtuka, alisikia furaha yenyi kupita yote, na akaona kama hii si ndoto. Pale pale alisadiki na roho moja, akamfuata Bwana Yesu kote alikokwenda, akajitolea yeye wote mzima kwake, na hata aliwavuta ndumba wengi akawapeleka kwa Bwana Yesu na kuwageuza. Aliacha mambo yake yote ya dunia.

— Wababa na wamama, tunasikia hali Maria Madeleine aliyokuwa nayo mbele. Basi mafundisho haya ya Maria Madeleine yanatufundisha nini? Tunaona kama tamaa mbaya ya Maria Madeleine iliponyeshwa na neema ya Mungu.

Pale alipokuwa akizungumza naye, hakuficha ubaya wake, kwa maana aliona hana kosa. Na vile Bwana Yesu hakumfukuza alimsikiliza na alimsaidia ili ageuke. Na sisi, wababa na wamama, tunapoona wakosefu, tusiwafukuze, tusiwazarau, ila tuwasaidie kusikia mapendo ya kweli katika njia ya Mungu. Mungu mwenyewe atamsaidia na atapata kugeuka, kuliko kumfukuza na kumpoteza lote!

Kama vile Maria Madeleine alivyogeuka lote, bila kurudi nyuma, sisi pia tukigeuka na kumfuata Bwana Yesu, inafaa tuwasaidie marafiki wetu wote, wale tuliokuwa nao mu vitendo vyo upagano. Maria Madeleine aligeuka lote, alimfuata Bwana Yesu popote; sisi pia tujikaze kugeuka lote, tumfuate Bwana Yesu siku zote na popote, ili tusipate kurudi tena katika hali yetu ya zamani, ya upuuzi wa kipagano, usharati, ulevi, magomvi, wizi, majivuno na tamaa mbaya: ile yote tunayowaza tu kama ni mapendo.

- Maria Madeleine alizaliwa lote katika Jamaa ya Mungu sababu alikuwa na tamaa kubwa ya kumjua Bwana Yesu. Na sisi tuwe na hamu ile, tumfuate Bwana Yesu. Atatuzaa katika Jamaa yake ya kimungu. Maria Madeleine alijiwazia kumwingiza Yesu katika tamaa yake ya dunia; bali ni yeye aliyezaliwa katika mapendo ya Bwana Yesu.
Kumbe tujikaze, tusiingizwe wala kupelekwa na marafiki wabaya katika tamaa ya kidunia, lakini tuwazae sisi katika mapendo ya kweli ya Mungu.

- Nyumbani mwetu, kama mama hajageuka, ni sawa na Maria Madeleine wakati alipokuwa katika hali yake ya zamani. Sisi wababa, tujikaze kwa kumgeuza, awe Maria Madeleine wa sasa, mwenyi kujitolea na kumfuata Bwana Yesu lote.

- Wababa na wamama, Maria Madeleine aliingia kwa Bwana Yesu njia yake ya kwanza kwa kuwa alijitolea kwa Bwana Yesu wote na kwa lote. Na sisi, tunaingia njia yetu ya kwanza kwa Bwana Yesu kama tunajitolea sisi wote na lote. Kuzaliwa kwa Maria Madeleine katika Jamaa ya Bwana Yesu na Mitume wake, ndiyo njia yake ya kwanza. Maria Madeleine alipojitolea na kumpokea Bwana Yesu wote mzima, tamaa na mambo ya upuuzi zilikufa zote. Sisi pia tukimpokea Bwana Yesu wote mzima, tuishi naye, tutumike naye, tutembee naye, tuwe naye mu roho na mu mawazo yetu yote. Tusiwe tena na tamaa nyingine, lakini tuombe kujazwa mpaka na Bwana Yesu na Roho yake. Ni yeye atakayetusaidia kwa kututosha katika vishawishi vibaya. Kumbe tusali kila siku na tumwombe mtakatifu Maria Madeleine na Mama Bikira Maria

watusaidie na kutuombea kwa Bwana Yesu ili tuwe nao ka
Jamaa yao ya mbingu.

.. .. .. .. .. .. .. .. .. ..

## KUTAYARISHA WATOTO KWA KUINGIA KATIKA NJIA YA KWAN

Kiisha mafundisho hayo yote, tunawatayarisha watot
namna hii :

Kwanza tutaangalia kama wanabadirisha mwendo wao r
kujitolea nyumbani, kila mmoja kwa mwenzake, maana yal
kuonyesha uvumilivu, mapendo na tabia ya mkristu mwema
Tutawapasha ya kama wanapashwa kujichagulia baba r
mama mmoja (nyumba basi inachagua nyumba nyingine msi
zi), nao watawasimamia na kuwachunga na kuwasaidia ka
magumu yao yote. Wale baba na mama watawafuata wale wa
katika mwendo na vitendo vyao, mpaka mwisho wa maisha
Wasimamizi wale (nyumba msimamizi) watachaguliwa kati
wababa na wamama wa njia ya tatu.

Wale wenyi kutaka kuingizwa katika njia ya kwanza
napashwa kuwa waaminifu na kutolea waziwazi mawazo ya
kwa wasimamizi wao. Mbele ya kuingizwa katika njia il
baba atatolea mawazo yake yote kwa baba msimamizi wak
atamwelezea mema na mabaya yote aliyotenda tangu utot
ke mpaka leo; na mama atafanya namna moja kwa mama ms
mizi wake. Hivi itawasaidia sana baba yule na mama yu
wasimamizi, kwa kuwaongoza watoto wao katika maisha y
yote. Na kama vile watoto walivyofanya kueleza mawazo
mbele ya wasimamizi wao, wasimamizi wenyewe nao pia w
eleza mema na mabaya waliyotenda katika maisha yao.

Kiisha tutawapa sala ya kusali muda wa siku kenda
Mungu apate kuwaangazia ili wawe umoja naye kila siku
Katika sala ya siku kenda, tunawapa pia wasali ile sa
yetu kubwa ya kama: "Bwana Yesu, unipe Bikira Maria;
kira Maria, unipe Bwana Yesu aniangazie, anitakase na
nitosha katika giza ya shetani na mitego yake yote.."

Kama sala hizi zinaisha, tutawaelezea sasa waende
jifanya umoja kati yao, baba na bibi wake wenyewe, ka
vile walivyojifanya umoja na wasimamizi wao wakiambia
mambo yao yote. Maana yake, baba amwelezee bibi yake
na mabaya yote aliyoyatenda tangu utoto wake; na mama
atafanya vilevile kwa bwana wake.

Mbele ya kuwatuma baba na mama waende kujifanya umoja tunawaletea angalisho ya kama wakati wa kutoleana mawazo, mume kwa mke wake, wawe na huruma kubwa sana, mmoja kwa mwenzake; wasitoshe upanga, lakini wakumbuke sala ya "Bab ba yetu" tuliyofundishwa na Bwana Yesu mwenyewe. Yule ata kayekosa huruma kwa mwenzake, Mungu basi hatamhurumia, na atampa malipizi. Tunawaomba pia wabebe roho ya Mungu Baba - ndiyo huruma -, roho ya Mungu Mwana, ndiyo roho ya ku - pokea; na roho ya Mapendo yenyi kuunganisha na kuchunga umoja wa Roho Mtakatifu.

Wakiisha kujifanya umoja, sasa wanapashwa kwenda kuun gama kwa Padri kusudi wapokee huruma ya Mungu.

Kiisha kuungama kwa Padri, watafundishwa mafundisho y Malaika Gabriel anayempasha Bikira Maria Habari.

.. .. .. .. .. .. .. .. .. .. ..

## IX.- MALAIKA GABRIEL ANAMPASHA BIKIRA MARIA HABARI. (Lk 26-

Siku moja Bikira Maria alikuwa chumbani mwake, katika nyumba ya wazazi wake; milango na madirisha ilikuwa yenyi kufungwa. Bikira Maria mara alishtuka: akaona kijana mwa- naume mzuri sana ameisha kuingia. Pale Bikira Maria akawa za na kujiuliza: "Huyu kijana anatoka wapi? Anafuata nini Bikira Maria akasikia woga sana. Kumbe kijana yule hakuwa mtu wa dunia, lakini alikuwa malaika Gabriel aliyetumwa na Mungu kwa kumpasha habari njema ya kumzaa Mkombozi. Na malaika akamwamkia na kusema: "Nakuamkia, Wewe unaye- jaa neema, Bwana ni nawe." Malaika akaongeza na kusema : "Usiogope, Maria, mimi natumwa na Mungu kwa kukuambia ya kama ukisadiki, utapata mimba na utazaa mtoto mwanaume; utampa jina lake Yesu. Atakuwa mfalme na kuitwa mwana wa Aliye-juu. Mungu atampa kiti cha baba yake Daudi. Atatawa la katika kizazi cha Yakobo milele, na ufalme wake hutaku wa na mwisho."

Maria alipokwisha kusikia hayo, akajibu: "Mambo haya yatatimizika namna gani? na mimi sijui mwanamume!" Malaik akasema: "Maria, usiwe na shaka; Mungu mwenyewe atashuka, atakushukia, nguvu ya Roho Mtakatifu itakufunika, na kwa uwezo wake utapata mimba. Angalia Elizabethi, dada yako, amepata mimba katika uzee wake, na inakuwa sasa miezi sita."

Maria akajibu:" Mimi mtumishi wake Bwana, nipate vyosema."

Halafu Malaika akapotea na kwenda zake.

Kwa kuwa Maria alikubali na kuitika maneno yale, shinda shetani, na kizazi chake -ndiye Yesu- kilivun chwa chake.

Saa ileile Mungu Mwana akaingia katika tumbo lak mawazo yake yote : ya ubaba, ya umwana na ya mapendo umoja. Bikira Maria alijazwa na furaha pa kuona kama bozi aliisha kuja duniani.

Na sisi pia, wababa na wamama, tunapashwa kumzaa kati yetu na kumsaidia kuwakomboa watu wote.

Hakuna namna ya kufasiria na kusikilizisha vema ile ginsi ilikuwa. Yale yote Mungu aliyomuwazia Biki ria inatimizika leo: mbingu na dunia na vyote vyenyi wamo, vyote ni vyake yeye aliye Mama wa Mungu.

Ile yote Bwana Mungu aliyomtendea Bikira Maria, aliichunga sana moyoni mwake, kama siri yake kubwa.

– § – § – § – § – § – § –

## KUINGIZA KWENYEWE

1. Baba na mama watakaoingia katika njia ya kwanza w toleana mawazo yao tangu utoto wao na kufikisha l Maana yake ni kufasiriana maisha mazima, uwema na ya wote, uzao na mawazo yao. (Wasitoleane mpaka m tu: si maungamo; ukomo ni kujuana kabisa.)
2. Wale wanaowafundisha wanawapa sala ili Mungu awac watoto hawa watatolea mawazo yao katika nyumba ga nyumba gani itawasimamia? Ni kuomba zaidi Roho Mt fu awaangazie; (na si kwa njia ya ndoto tu: wengi hawapati ndoto). Mungu anatumika kwa njia nyingi namna mbalimbali. Wanapashwa kuwaza mapendo yao i sukuma wapi. Muchunge pia n° 16 ya kanuni za Jam "Baba ao mama anayekuwa tayari kwa kuingia katika ya kwanza yupo na uhuru wa kuwachagua baba ao man msimamizi. Asilazimishwe kuchagua baba ao mama fu tu."
3. Kiisha kutoleana mawazo, wanafuata n°17 ya kanuni Jamaa: "Wababa na wamama walio tayari kwa kupata yao ya kwanza ao ya pili ao ya tatu wanapashwa ku shwa katika mkusanyo wa wababa na wamama wa njia

unaofanyikwa mara moja kila mwezi. Humo watapewa mashauri yenyi kuelekea njia yao."
Wale wanaowaendelesha wanawapa sala: sala ya sikitik sala ya kusadiki na ya kitumaini, 'Baba yetu' mara tatu, 'Nakuamkia Maria' mara tatu, na 'Sifa kwa Baba' mara tatu. Sala ile wataisali siku kenda. Wakati ule, wababa na wamama wote wanaungana nao katika sala.

4. Baba na mama watakaoingia katika njia ya kwanza wanatolea mawazo yao kwa wale wanaowasimamia.
5. Wale wanaowafundisha wanasikilizana na Padri atakayewaingiza, wapate kujua wataweza kuonana naye siku gani. Pale Padri atazungumza nao apate kujua namna waligeuka, na sasa mawazo yao ni ya namna gani, kama mwendo wao, ndoa yao, maisha yao mazima yaligeuka kwa nguvu ya Roho Mtakatifu kuwa maisha na mawazo ya Bwana Yesu kwa sifa ya Mungu Baba.
6. Kwa desturi, ni Padri wa Paroisse yao atakayewaingiz tukifuata n°19 na n°20 za kanuni za Jamaa. Lakini msilazimishe Padri wa Paroisse; akiwa anakataa, msikilizane na Padri mwengine anayeitikia kazi ile, na mumpashe habari Padri wa Paroisse ya kama baba na mama fulani wataingia katika njia yao ya kwanza.
7. Kiisha kuzungumza na Padri atakayewaingiza katika njia ya kwanza, wanasikilizana juu ya siku gani wataingia katika njia ile.
8. Kwa kuingia: mama anayeingia atasindikizwa na Mama mwenyi kumsimamia;
   baba anayeingia atasindikizwa na Baba mwenyi kumsimamia.

   (Mashahidi, baba ao mama, mmoja ao wawili wanapata ruhusa ya kuwapo.)

Padri anauliza- kwa Baba (mtoto): "Unamjua Baba huyu?
Mama Mama
Unamjua kabisa(msimamizi) vile anavyotembea na mawazo yake yote?"

Kiisha yake, Padri anauliza tena:
- kwa Baba (msimamizi): "Unamjua mtoto wa-
Mama
ko? Unamjua kabisa vile anavyotembea na mawazo yake yote?"

Kiisha Padri anasema: "Ikiwa mnavyojuana vile, uliisha kusikia ao kuzungumza juu ya umoja wa Bikira Maria na Bwana Yesu. Bwana Yesu

alikuwa baba, mwana na mapendo kabisa kwa Bikira
ria; Bwana Yesu alijitolea kabisa kwa mama yake.
Bikira Maria alikuwa mama, mwana na mapendo kabi
kwa Bwana Yesu; Bikira Maria alijitolea kabisa k
Bwana Yesu.
Kama Bwana Yesu (ao Bikira Maria) anakupa Bikira
(ao Bwana Yesu) kuwa Baba (ao mama), Mwana na Ma
kwako, kumbe kati yako na yeye kutakuwa mipaka t
Si kutakuwa urafiki wa kweli, na undugu wa kweli
ya wewe na wao.
Kama ni vile, wewe mama (ao baba) uende kusali s
sikitiko juu ya makosa yako yote uliyotenda tang
to wako, na ukasali 'Baba yetu' mara tatu, 'Naku
Maria' mara tatu, na uombe: "Ee Bwana Yesu, unip
kira Maria; ee Bikira Maria, unipe Bwana Yesu."

Kiisha yake, Padri anampa baraka (alama ya msalaba
ya uso wake na kumwekea mkono.
Kiisha yake anawatuma kwao; waende na heshima na a
yote kusali na kuwaza.

9. Wababa na wamama wanaoingia kwa Padri fulani wanap
kubaki naye katika umoja : kusali pamoja naye, kuz
gumza pamoja naye na kutoleana mawazo.

+o=o+o=o+o=o+o=o+o=o+

Bwana Yesu akasema :

"Je, hamkusoma kama yule aliyemwumba mtu
tangu mwanzo amewaumba mume na mke?
Naye amesema :
'Basi mtu atawaacha baba na mama
ataungana na mke wake.
Wawili watakuwa mwili mmoja.'
Hivi si wawili tena, bali mwili mmoja tu.
Kilichounganishwa na Mungu,
mtu asikitenganishe."

Mateo 19,4-6

Mafundisho ya Jamaa

## + NJIA YA PILI +

Bwana Yesu akasema tena :

"Mtu anayekuja kwangu, bila kunipenda
kupita baba yake na mama yake,
na mke wake na watoto,
na ndugu yake na dada,
na hata uzima wake,
hawezi kuwa mfuasi wangu...

Nani kati yenu, akitaka kujenga nyumba,
hakai kwanza apate kuhesabu bei ya kazi,
na kuona kama makuta yake yataenea kwa kuitimiza'
Kwa maana akiweka misinji tu, asipoweza tena
kumaliza, watu wote watakaomwona wataanza kum-
chekelea wakisema: "Mwangalieni huyu, alianza
kujenga, hakuweza kumaliza."

Luka 14,26-30

Njia ya pili, MAANA YAKE.

"Njia ya pili" ni ukumbusho wa Ndoa ya Kikristu (sa
menta ya ndoa). Ni umoja wa baba na mama katika ndoa ya
pamoja na Mungu kati yao.

Baba bila mama, ao mama bila baba, hatuwezi kumwing
katika njia ya pili; lakini - akitaka mwenyewe - atapew
mafundisho yote ya njia ya pili.

1/ BIKIRA MARIA KWA ELIZABETHI. (Luka 1,39-56)

Kama vile alivyoambiwa na Malaika Gabriel, Maria ak
da kumwangalia dada yake ya tumbo lingine, jina lake El
bethi. Maria akawaaga wazazi wake ya kama: " Naenda kwa
dada Elizabethi." Akafunga safari, akaenda. Wakati alip
ka kwa dada na huyu alipomwona, Elizabethi akajaliwa na
Roho Mtakatifu na akasema kwa sauti kubwa: Mbarikiwa we
kuliko wanamake wote, na mbarikiwa mtoto wa tumbo lako.
Palepale mtoto akarukaruka tumboni mwa Elizabethi, na y
wa mu tumbo la Maria akarukaruka na furaha vilevile. Na
mama Maria akamshukuru Mungu na kumwimbia wimbo wa "Mag
ficat."

Wababa na wamama, pale Maria aliposikia maneno ya E
zabethi, alihakikishwa juu ya yale yote aliyoambiwa na
Malaika wa Mungu, na kutimiliza mapashwa tale aliyoambi
tena kwa kwenda kumsaidia Elizabethi... Kumbe na sisi t
me kufuata mfano wa Bikira Maria kwa kuonyesha utii mbe
ya Mungu na kusaidia watu wenzetu. Ukiwa mkubwa kwa kuz
liwa, ku kazi ukiwa na cheo ao bila cheo, ufuate mfano
Bikira Maria, hivi utampendeza Mungu na watu wote.

2/ SHAKA YA YOSEFU NA NDOA YAO. (Mateo 1,18-24)

Bikira Maria alipokwisha kumsaidia dada yake Elizal
thi, akarudi nyumbani mwa wazazi wake. Mchumba wake Yos
alipopata habari ya kama Maria mchumba wake ana mimba,
akasikitika sana, akakata tamaa na akawaza kumkataa Ma
Lakini Yosefu alikuwa na huruma juu ya Maria ya kama :
"Nikimtoa mimi, Maria atauawa na wazazi wake, wataazifi
vikali." Halafu Yosefu akatafuta mayele katika uficho,
kwenda kuchukua mali ake, kukimbia zake. Alipokuwa aki
za hivyo, Mungu akamtumia malaika, katika ndoto, kwa ku
mwambia kama: "Yosefu, usikatae kwenda kumbeba Maria,

mke wako; mimba ile unamwona nayo, si ya mtu, lakini ni nguvu ya Roho Mtakatifu iliyomfunika apate kumzaa mtoto wa Mungu. Ni yeye atakayekuwa Mkombozi wa dunia nzima." Na Malaika akaongeza, akamwuliza Yosefu: "Unapenda vile kumbeba bibi na mimba isiyokuwa yako, kumchunga kabisa kabisa, bila msito na hasira, mpaka atakapozaliwa Mkombozi; halafu utawachunga wote, Bikira Maria na mtoto Yesu, na kutimiza kazi yako ya ulinzi?"

Yosefu aliposikia hayo, akasadiki yote na roho moja, bila shaka.

Malaika akaendelea tena, akasema: "Uende; ukambebe Maria, umchunge na umpende na mapendo yote tatu: utampenda na mapendo ya umwana kwani Maria ni mama yako, na mapendo ya ubaba kwani Maria ni mwana wako; utampenda na mawazo ya umoja kwani Maria ni bibi yako, lakini utaheshimu mwili wake kwani ni Mama wa Mwana wa Mungu.

Bikira Maria, ngambo yake, naye alikuwa na masito. Alikuwa na masito. Aliwaza na kujiuliza ya kwamba: "Sasa hivi nakuwa na mimba, Yosefu atakubali kunioa tena mimi? Si atanikataa akisema: 'Unakuwa na mimba nisiyojua kule inakotoka!' Nitamwambia nini? Kama ananikataa, nitafanyaje? Nitabaki tu mpaka na Mungu!"

Bikira Maria akiwa anahangaika namna hii, Yosefu anamwambia: "Malaika wa Mungu alionekana kwangu na aliniambia maneno yako yote." Na Yosefu alimpokelea, na kumpenda, na kumheshimu. Basi Bikira Maria anaona kama Yosefu mtakatifu aliisha kutulizwa na Malaika wa Mungu, na yeye vilevile akaitika kumpenda Yosefu na mapendo yote tatu, na akamwambia Yosefu: "Nitaishi nawe katika umoja wa mapendo yote tatu: nitakupenda na mawazo ya umama kwani wewe, Yosefu, ni mwana wangu; na nitakupenda na mawazo ya umoja kwani wewe, Yosefu, ni bwana wangu; na nitakupenda na mawazo ya umwana kwani wewe, Yosefu, ni baba yangu."

Tangu pale, Maria hakuwa tena na woga. Yosefu akaja kumchukua, kama vile Malaika alivyomwelezea, na wakaunga ndoa yao. Akabaki naye bila kumwazia ubaya wowote, akamchunga vema, wakasikilizana na kusaidiana katika maisha yao yote. Walipendana katika mapendo ya kweli na ya milele

Basi, wababa na wamama, neno kubwa la kusadiki na Imani kubwa, bila masito, ni hili : Yosefu alimpenda na kumpokea Maria katika maisha yake yote, kama bibi yake, lakini hakuujua mwili wake vile wabwana wote wanavyojua mabibi wao. Kwake aliona na kusikia waziwazi mashauri ya

Malaika na ya Mungu; ile ilimfikia katika ndoto, ni ile Eklezya mama yetu anayotufundisha, ya kama: Yosefu ni b mlinzi tu wa Bwana Yesu. Kumbe kwa kuwa tupo waaminifu Mungu, yafaa tuwe watii katika mafundisho yake, kama vi Yosefu na Maria walivyosadiki yote, bila kutaka kujua w ziwazi.

Tuwe wapole, wavumilivu, na wenyi huruma kwa wenzet watakapokosea. Tuchunge na heshima kubwa neno la Mungu. Tuwe na Imani kubwa, kama vile Yosefu na Maria, kwani M gu hatuwezi kumwona na macho na kumkamata na mikono. La ni Mungu wetu tunamwona tu kwa macho yetu ya ndani, ya ho. Ni ile Imani yetu ya kweli!

## 3/ KUZALIWA KWA BWANA YESU BETLEHEMU. (Luka 2,1-20)

Kiisha karamu ya ndoa, Yosefu na Maria wakaishi na endelea pamoja kazi yoa yote: Yosefu alitumika katika k banda chake cha usermala, na Maria alitayarisha kazi yo ya nyumba: kupika chakula, kusafisha mavazi, kupamba nj ba yao, na vivi hivi.

Mwaka ule ule, mfalme mkubwa wa Roma alileta amri y kuhesabu watu wote wa nchi yake; na kila mtu alipashwa kwenda kujiandikisha mpaka katika nchi yake ya kuzaliwa Yosefu na Maria, kwa kuwa Yosefu alikuwa wa kizazi cha Daudi, walipashwa kwenda Betlehemu, mji wa kuzaliwa wa bo yake Daudi, ili waende kujiandikisha kule.

Safari ilikuwa ndefu sana na ya milima. Maria, kwa wa mimba yake imekwisha kukomea, na kulikuwa mwezi wak kuzaa, alichoka sana kwa safari ile; na wakafika Betle Kiisha kufika kule, walitafuta fasi ya kulala [illegible] hawakupata sababu watu walikuwa wengi mno, na nyumba z zilijaa. Lakini Yosefu, kwa kuwa alikuwa mtu wa zamani pale Betlehemu, alipata mawazo ya kwenda kuangalia pem ya mji, kule wanakolishia wanyama, kama watapata fasi. hivi walienda kupata nyumba moja ya kulishia wanyama, walingiamo. Wakatengeneza fasi yao ya kulala. Hapo us kati, mtoto wa Mungu, Mkombozi wa watu, akazaliwa, pas matata wala maumivu yoyote kwa mama, hata kuzaliwa bil kuharibu mwili wa mama yake; na mama Maria alibaki na kira wake, kama vile alivyokuwa tangu mwanzo mpaka leo

Kiisha kuzaliwa kwa mtoto, Yosefu na Maria walifur sana na wakapiga magoti mbele ya mtoto, wakamshukuru M Halafu wakasikia malaika wanaoimba:"Sifa kwa Mungu mbi na amani duniani kwa watu anaowapenda."

Habari ile ilipelekwa pia na malaika kwa wachungaji ya kama: "Nendeni Betlehemu ya Yuda, huko Mkombozi wa dunia amezaliwa. Mtamkuta mtoto aliyevalishwa mavazi ya kitoto na amelalishwa katika sanduku ya kulishia wanyama."

Wachungaji walienda kwa upesi sana, wakamkuta mtoto kama vile walivyoambiwa na malaika, wakapiga magoti mbele yake, na kumwabudu, na kumtolea sadaka yao.

Wababa na wamama, tukiwaza vizuri, tutaona kama Bwana Yesu anatupatia kifupi cha kazi yake kubwa ya ukombozi. Tutapima kuisikiliza namna hii:

Bwana Yesu ni Mungu wa uwezo wote, na kama angetaka, angeweza kusaidia Yosefu na Maria kwa yote, kusudi wafike mbele ya wengine wote, pasipo kuchelewa. Hata angeweza kutuma mawazo yake katika nyumba fulani, kusudi waache fasi moja, kwa kuwa kutafika bwana na bibi. Lakini Bwana Yesu hakupenda kufanya ile yote, sababu: Bwana Yesu alitaka kutufundisha hapa unyenyekevu, kwa kujionyesha mbele ya watu wote kama vile mtu wa bure...

Alituonyesha pia kama njia yake ni ya mateso, si ya furaha na ya sifa.

Alikataa kuzaliwa nyumbani mwa watu wengine kwani aliona kama hamuna umoja, mapendo na masikilizano. Alipenda kuzaliwa nyumbani mwa Yosefu na Maria, kwa sababu mulikuwa umoja, masikilizano na mapendo kuliko wengine.

Alizaliwa usiku kati, kwani ni wakati wa ukimya. Yeye ndiye ukimya, na analeta amani duniani.

Hakuharibisha mwili wa mama yake, ndiyo alama kubwa la umungu. Na mtoto mwema anachunga roho na mwili wa mama yake.

Basi, wababa na wamama, tunasikia mambo yote ya kuzaliwa kwa Bwana Yesu. Tunaona kama yote ilipita tu katika umaskini. Kumbe sisi vilevile inafaa tuwe na mapendo ya kweli, pasipo uchaguzi ao kuwapenda tu watajiri. Tupende watu wote, hasa wale wamaskini. Tupende pia kujifanya wanyenyekevu, wamaskini, na kujishusha mbele ya wengine. Tunapashwa vilevile kuwa na mapendo makubwa kwa wazazi wetu, kama vile Bwana Yesu alivyotuonyesha heshima na mapendo kwa wazazi wake. Tuwe na heshima na mapendo makubwa katika nyumba zetu : baba, mama na watoto. Tukifanya vile, kweli, wababa na wamama, tutamzaa Bwana Yesu nyumbani mwetu!

4/ KUTAHIRIWA KWA MTOTO YESU. (Luka 2,21)

Kama vile ilivyokuwa zoezo la Mayahudi, kila mtoto mwanamume alipashwa kutahiriwa kiisha siku nane ya kuza wa kwake. Mtoto Yesu naye, kwa kuwa alikuwa Myahudi, a hiriwa siku ya nane ya kuzaliwa kwake, na alipewa jina ke Yesu, kama vile alivyoambiwa na Malaika.

5/ KUTOLEWA KWA MTOTO YESU HEKALUNI NA KUTAKASWA KWA BIKIRA MARIA. (Lk 2,

Kama vile tulivyosema mbele, Bwana Yesu alitaka ku ta kanuni zote za nchi yake, na basi alitolewa hekalun kama vile desturi ya Mayahudi ya kutolea mtoto mwanamu aliyezaliwa wa kwanza ku kila kizazi, kwa kuwa zawadi Mungu. Kitendo kile kilikuwa ukumbusho wa kanuni ya Mu kwa kumshukuru Mungu, sababu ya kutoshwa kwao katika u wa Misri.

Yosefu na Maria waliingia hekaluni na wakamtolea m Yesu kwa Mungu, katika mikono ya Mkohani mkubwa. Kulik pa Yerusalem mtu mmoja jina lake Simeon. Siku ile akaf hekaluni, na alipomwona mtoto, akampokea na kutambua k ni yeye Masiha, Mkombozi wa watu; akamshukuru Mungu na sema: "Sasa, Bwana, unaweza kuacha mtumishi wako aende amani, kwani macho yake yanamwona Mkombozi yule tuliye ngoja siku nyingi!" Kiisha akamwangalia Maria; akasema "Mtoto huyu si wako peke, ila alikuja kwa ukombozi wa nia nzima. Moyo wako utachomwa kwa upanga na uchungu, utakapomw na mtoto wako kuteswa kwa ajili ya watu wote

Halafu Simeon akamwonyesha mtoto kwa watu wote. Ak disha mtoto kwa mama yake.

Katika sheria ya Musa, kila mwanamke Myahudi, akii kuzaa , na ikipita siku makumi manne, alipashwa kwenda takaswa. Basi siku ileile ya kutolewa kwa Yesu hekalun Bikira Maria alitakaswa, kwa kumaliza yote yaliyoamriw Bwana. Yosefu na Maria wakatolea sadaka yao ya njiwa w , kama ilivyoandikwa katika sheria ya Mungu, kwa kukom mtoto.

Mule ndani ya hekalu, kulikuwa pia mama mzee na mt fu, jina lake Anna, naye alikaribia Yosefu na Maria, a mwona mtoto. Alifurahi na kumsifu Mungu.

Wababa na wamama, tunasikia katika mafundisho haya kama Bwana Yesu, kwa kutaka kutimiza kazi yake ya ukom alibeba umuntu wetu wote, apate kuishi pamoja na mtu k

kumkomboa. Yeye, kwa kuwa ni Mungu, hakuwa na lazima ya kutahiriwa wala kutolewa hekaluni, lakini aliitimiza tu kwa kutaka kutuonyesha mfano wa unyenyekevu na utii kwa Mungu na kwa wakubwa wa nchi. Kumbe sisi vilevile, tufua mfano ule wa Bwana Yesu. Tusiseme: "Mimi niko mtu wa Mun siwezi kufuata na kutii amri za wakubwa wa nchi", na kuz rau ndugu yetu kama wale ni 'wa mwili'. Lakini tuangalie vema amri za wakubwa wa nchi, tunapashwa kuzitii ikiwa z napatana na zile za Mungu. Zikiachana na vile Mungu ana-vyotaka, pale hatutatii, kwani tunapashwa kuogopa Mungu kuliko watu wa dunia.

Tunaona tena, wababa na wamama, namna Bwana Yesu ana-vyopata jina lake, na tunaona pia maana yake. Na sisi pi wakati tunapobatiza watoto wetu, tusikie vizuri maana ya jina lile tunalowapatia: wako watoto wa Mungu, wako mali yake. Na tujitayarishe vizuri kwa siku ile ya kuzaliwa kwao katika uzima wa Mungu, si kwa karamu ao feti tu, la-kini na zaidi kwa sababu watoto wetu wa mwili wataanza kuwa watoto wa Mungu pia.

6/ <u>MAJUSI WATATU WANAKUJA KUMWABUDU MTOTO YESU.</u>(Mt. 2,1-

Kiisha kuzaliwa kwake Bwana Yesu, habari ilifika pia katika nchi ya mbali. Kule wafalme watatu wa nchi mbalim li waliona nyota ya namna **ya pekee** mbinguni. Waliposoma katika vitabu vyao, wakatambua kama ni alama ya kuzaliwa kwa Mkombozi. Palepale, kila mmoja akatoka katika nchi yake, akafuata nyota ile kwa kwenda kumwona mtoto Mkombo

Njiani, wote watatu wakakutana na kuongeza safari. W kafika katika mji wa Yerusalem, wakauliza kwa wakaaji: "Ni wapi alizaliwa mfalme mpya wa Mayahudi?" Watu wale hawakujua habari ile. Halafu Herodi akawaita wakubwa wa dini, akawauliza juu ya habari ile. Wale walienda kusoma katika vitabu vyao, na wakamjibu mfalme Herodi kama ni kweli, wakati uliosemwa umetimia: "Inawezekana kama ame-zaliwa ku Betlehem ya Yudea." Herodi aliposikia hayo aka-shtuka sana, na akawaelezea Majusi akisema: "Nendeni Bet hem, na mkiisha kumwona mfalme yule aliyezaliwa, mrudie na kunielezea, na mimi pia niende nikamwabudu."

Wakati Herodi alipokuwa akisema hivyo, si kwa mapend lakini ni kwa chuki tu, na mawazo ya kutaka kumwua.

Majusi walitoka Yerusalem, mara wakaona tena nyota i iliyowaangazia, mpaka walipofika ku nyumba walikokuwa

mtoto Yesu, Maria na Yosefu. Majusi walimwabudu mtoto
na wakamtolea zawadi zao za zahabu, ubani na manemane
Zahabu, maana yake "maombi yetu ikufikie kama vile mo
na harufu nzuri"; na manemane, maana yake "tunakuhoin
kukutolea mapendo yetu yote; zahabu maana yake "uko m
mkuu wa mali yote."

Majusi walipotaka kurudi katika nchi zao, Malaika
Mungu akawatokea usiku, katika ndoto, na kuwaambia: "
di kwa Herodi, kwani anataka kumwua mtoto." Asubui, M
walirudi kwao, wakipita katika njia nyingine.

- Wababa na wamama, mafundisho haya ya Majusi yan
sha kama Bwana Yesu hakuzaliwa kwa ajili ya watu wa k
moja tu, ila kwa watu wote! Ni ile tunayoona katika t
ya Noeli: mfano wa watu watatu wa rangi mbalimbali.

Majusi walitoka katika nchi za mbali na kumfuata
Yesu. Nyota iliwaangazia Majusi na kuwaonyesha njia.
sisi, nyota yetu ni Eklezya inayotuonyesha njia na ku
leka kwa Bwana Yesu.

Herodi alishikwa na chuki na kutaka kumwua mtoto
Sisi tunapashwa kuogopa kuchukia wenzetu, kwani ni ha
ya kupotea.

Tukitoka ku Misa ao ku mafundisho ya Mungu, tunap
kumchunga Bwana Yesu rohoni mwetu na kumwepusha katik
tari zote. Kwa mfano: hatari ya kushinda katika "ma-
ao ya kutembea na marafiki mabaya...

## 7/ KUKIMBILIA MISRI (Mateo 2,13-18)

Herodi alipoona kama siku nyingi zinapita na Maju
hawafiki kwake, akashikwa na woga na akawaza kama ku
mtego kwa kutaka kumnyanganya cheo chake. Halafu aka
namna yote ya kumwua mtoto. Aliita wafuasi wake na ku
liza juu habari ya mfalme yule mpya, lakini hawakupat
tambua nafasi ile yupo wapi. Kiisha Herodi alitoa am
kuwaua watoto wachanga wote waliozaliwa katika mwaka
mpaka na wale waliokuwa na umri wa miaka miwili, kati
mji wa Betlehem na kandokando yote.

Mungu alipoona mawazo yale mabaya ya Herodi, aka
Malaika kwa kumpasha Yosefu wakimbie na mtoto. Malaik
fika kwa Yosefu katika ndoto, akamwambia: "Kamata mt
pamoja na mama yake, mukimbilie ku Misri; mtabaki ku
mpaka nitakapowaelezea, kwani Herodi anamtafuta mtot
kumwua."

Palepale Yosefu akaamka, akamwelezea Maria, na wakati ule ule wakafunga safari na kukimbilia Misri. Njiani kwa kwenda Misri waliteswa sana, kwani safari ilikuwa ndefu mno. Walitembea usiku na mchana, kwa sababu waliogopa kama waaskari watawafuata...

Kule Btlehem, waaskari walienda kuwaua watoto wachanga wote wa mji ule na kandokando yake.

Wababa na wamama, kila mara, sisi watu wa Afrika, tunasema kama Bwana Yesu alikuja kwa watu wengine, lakini kwa sisi, hapana! Ni wongo! Tunaona katika mafundisho ya kukimbilia Misri kama Bwana Yesu na utoto wake wote alienda kuchungwa katika mji mmoja wa Afrika, kusudi asiuwe. Kumbe Bwana Yesu alikuja, si kwa kabila fulani tu, ila kwa watu wote.

Tunaona pia kama Bwana Yesu ni mfalme wa amani; hapend vita wala matata yoyote.

Basi hiyo inatufundisha sisi pia kama, katika nyumba yetu, baba na mama, tunapashwa kuwa na amani na ukimya. Tusitoe magomvi, matusi na kupigana kati yetu. Tukifanya hivyo, ni kutafuta namna ya kumwua Bwana Yesu katika nyumba yetu na kati yetu.

8/ KURUDIA KWA JAMAA NTAKATIFU NAZARETI. (Mateo 2,19-2

Jamaa ntakatifu ilibaki katika mji wa Misri siku nyingi sana. Na siku moja, Malaika akaja kumpasha Yosefu ya kama "Sasa, mrudi katika nchi yenu, kwani yule aliyetaka kumwua mtoto amekwisha kufa. Lakini msirudi tena Betlehem ila mwende tu Nazareti, sababu yule aliyemkomboa Herodi ni mtu mkali!" Yosefu na Maria basi walienda kukaa Nazareti, wapate kutimiza maandiko ya zamani yaliyosema: "Watamwita Mnazareti."

Nazareti, Jamaa ntakatifu ilikuwa mfano wa jamaa nyingi: Yosefu alijitolea sana katika kazi yake ya usermala, ili apate kulisha, kuvika na kutunza Maria na Mtoto wao; alimtii sana Maria na kumfanyizia yote ili ampendeze. Al wachunga sana mu vyote. Basi alikuwa mfano wa wanaume wo

Maria alikuwa mfano wa wanawake wote. Maria alijitol na roho na nguvu zake zote kwa kutumika kazi yote ya nyumba, apate kulisha Yosefu na Mtoto.

Yesu naye alionyesha umwana wake na utii mkubwa sana mbele ya wazazi wake katika kazi yao yote. Alimsaidia Bikira Maria kwa kazi ya nyumba, sawa na kufagia, kushota

maji, kubeba kuni, na vivi hivi. Na kwa Yosefu pia ali
saidia kila mara katika kazi yake ya usermala.

Yosefu na Maria walimwadibisha mtoto Yesu; na yeye
alijishusha mbele yao, akiwaonyesha utii na mapendo ya
